Jumatano Juni 9, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

ISSN 0856 • Na. 0580606

www.ippmedia.com

MWANGA WA JA

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US

**Rais** Samia amlilia Mzindakaya, kuzikwa mjini Sumbawanga

UKURASA 5



**Serikali** yasitisha vibali vya uagizaji sukari nje ya nchi

UKURASA 5



**Koeman kastahili kupewa mwaka Barca - Guardiola**

UKURASA 20

# UKOMBOZI WANAWAKE

• **Shule** za sayansi wasichana kila mkoa, aja na mpango kabambe kuwawezesha kiuchumi, teknolojia... *Endelea ukurasa 2*




Rais Samia Suluhu Hassan akizungumza na wanawake wa Tanzania, jijini Dodoma jana. **PICHA: IKULU**

## Mashamba mengine 86 ya vigogo kutaifishwa

UKURASA 3



## RC Makala aweka bayana vipaumbele Dar es Salaam

UKURASA 3

**MICHEZO** **TARIMBA ATINGISHA KUGOMBEA URAIS TFF** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6




Ofisa Mkuu wa Wateja Binafsi na Biashara wa Benki ya NMB, Filbert Mponzi (kushoto), akikabidhi mkataba kwa Mkurugenzi na Mkuu wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), Bernard Konga, baada ya kutiliana saini mpango wa Bima ya Afya kwa wakulima wa vyama vya ushirika kwa uhakika wa huduma za matibabu wakati wote na popote, jijini Dar es Salaam jana. Katikati ni Naibu Mrajis wa Vyama vya Ushirika, Udhibiti na Usimamizi wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika (TCDS), Collins Nyakunga. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Shule sayansi wasichana sasa kujengwa kila mkoa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

RAIS Samia Suluhu Hassan amesema mpango wa serikali kujenga shule za sekondari za wasichana kwa ajili ya masomo ya sayansi kila mkoa, utaanza kutekelezwa mwezi ujao.

Amesema ujenzi wa shule hizo utasaidia kufikia malengo ya usawa wa kijinsia wa 50 kwa 50 kwa kuwa wanawake bado wako nyuma kwenye masomo ya sayansi.

Akizungumza jana na wanawake Dodoma, Rais Samia alisema dunia ya sasa inaendeshwa kwa mifumo ya kidigitali na utafiti unaonyesha kuna pengo kubwa kwenye matumizi ya mifumo hiyo kati ya wanaume na wanawake.

"Wanaume wanaonekana ni wepesi kwenye matumizi ya mifumo hii kuliko wanawake na hii mifano ipo hata kwangu mimi. Nikikwama kitu kwenye simu yangu kitu kidogo kuna kajukuu kangu kanaitwa Ibra, ukimwambia hebu chukua simu yangu itizame. Ana miaka tisa, anachukua anaangalia ananipa tayari, kasomeshwa na nani, anajua Mungu.

"Lakini nina mjukuu anaitwa Samia namwita njoo niangalizie hii simu ina tatizo gani ananiambia bibi mimi sijui ngoja nimuite Ibra. Watoto wa kiume wako haraka kushika zaidi kuliko wa kike," alisema.

Kutokana na hali hiyo, alisema serikali imefanya uamuzi wa kujenga shule hizo za wasichana kwa ajili ya masomo ya sayansi ili kuziba pengo la kidigitali na kufikia mapinduzi ya viwanda.

"Leo hii unawakuta wavulana wapo vibandani wamejiajiri kwa kutumia mifumo ya kidigitali lakini watoto wa kike kuuza nyanya na michicha. Kwa hiyo tuna kazi ya kuziba hilo pengo. Lazima watoto wetu wasimame vizuri eneo hilo na serikali itaenda kusimama kwenye hilo," alisisitiza.

Alisema wasichana wanaanza wengi kwenye elimu ya msingi lakini kadri wanavyopanda idadi inapungua, hivyo wataangalia kitu gani kinasababisha na kukitatua. Pia alisema wanawake wanakabiliwa na vikwazo vingi kwenye mfumo wa elimu na kwamba serikali itaendelea kujenga miundombinu ili kuwaondolea watoto adha hizo.

"Julai mwaka huu tutaanza kutekeleza kwa kujenga shule moja ya sekondari yenye mabweni kwa kila mkoa kwa ajili ya masomo ya sayansi kwa wasichana, kwasababu Waziri wa Elimu ni mama sina shaka hili atakwenda nalo vizuri,"alisema.

Hata hivyo, Rais alisema hatua zimepigwa katika uwiano wa kijinsia kwenye eneo la elimu na kwamba idadi ya wavulana na wasichana kuanzia shule za msingi hadi vyuo vikuu inakaribiana.

"Kwa mfano shule za msingi zina zaidi ya wanafunzi 11, 200,000 na wasichana ni zaidi ya Sh.5,600,000 sawa na asilimia 50.4, kidato cha sita idadi ya wasichana sawa na asilimia 43.9, vyuo vya ufundi asilimia 47.8, vyuo vikuu asilimia 43 ni wasichana. Hali yetu siyo mbaya tunaongezeka," alisema.

**UWIANO WA KIJINSIA**

Rais alisema Tanzania imepiga hatua katika uwiano wa kijinsia kwenye vyombo vya uamuzi na ajira na kwamba idadi ya wanawake imeongezeka.

"Hivi karibuni nilipoingia kama Rais, nimefanya uteuzi wa makatibu tawala wa mikoa 26, hapa ndipo nilipofanya vizuri zaidi na sijui kama kuna eneo nitafanya vizuri zaidi ya hapa kati yao 12 wanawake sawa na asilimia 46, labda uteuzi wa pili kutakuwa na 50 kwa 50,"alisema.

Pia alisema kwa upande wa Mahakama ameteua majaji 28 wa Mahakama Kuu ambapo 13 ni wanawake sawa na asilimia 43.

"Hii 50 kwa 50 haipo mbali na idadi hii imeongeza kufikia 40 kati ya 86 waliopo,"alisema.

Aidha, alisema kwa upande wa Bunge kwa sasa ni kipindi cha pili kuwa na Naibu Spika mwanamke na idadi ya wabunge imeendelea kuongezeka kutoka 127 mwaka 2015 hadi 143 kwa sasa.

"Na kwa mara ya kwanza kwenye historia ya nchi nimeteua katibu wa bunge mwanamke na inanipa matumaini miaka michache ijayo tutafikia usawa wa kijinsia kwenye vyombo vya uamuzi,"alisema.

Pamoja na mafanikio hayo, alisema wanawake wengi hawapo kwenye ajira za mfumo rasmi ambapo asilimia 70 wapo kwenye ajira zisizo rasmi kama vile biashara ndogo ndogo, migodini, kazi za nyumbani.

"Kwa mujibu wa takwimu za mwaka 2017 kati ya watu milioni 3,014,106 waliokuwa kwenye ajira rasmi wanawake walikuwa 1,100,900 sawa na asilimia 36.8. hali hii inasababishwa na mambo mengi ikiwamo majukumu ya kifamilia, hivyo kufanya waajiri hasa wa sekta binafsi kutopenda sana kuajiri wanawake," alisema.

# ...Amulika uchumi wa wanawake

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

RAIS Samia Suluhu Hassan, amebainisha kuwa ameunda kamati ya wataalamu watakaomshauri namna ya kuimarisha uchumi kwa wanawake nchini na Afrika.

Samia ambaye alitumia takriban saa 1:18 kuzungumza na wanawake jijini Dodoma, alisema dhamira yake na serikali ni kushughulikia masuala mbalimbali ya wanawake ikiwamo kuwainua kiuchumi.

Alisema wakati wa mkutano wa Afrika na Ufaransa ambao ulifanyika hivi karibuni ambao alishiriki kwa njia ya mtandao, alipewa heshima ya kuchagua eneo moja la kumjenga mwanamke ili lisimamiwe.

"Katika kikao kile nimeamua kuchagua eneo la haki za kiuchumi kwa wanawake kwa kutambua uwezeshaji wanawake kiuchumi ni nguzo muhimu ya kuleta usawa wa kijinsia hivyo nawaomba wadau tushirikiane katika hilo," alisema.

"Najua kati yetu kuna vijana wazuri kwenye mabenki ikiwamo ndugu yetu wa NMB ni mmoja wa wanawake watakaoshiriki kwenye hili, akiwamo Beng'i Issa (Katibu Mtendaji wa Baraza la Taifa la Uwezeshaji Kiuchumi) na wanawake wote waliopo kwenye sekta za kiuchumi watashiriki kwenye hili," alisema.

Alisema wataalamu hao watashiriki kuchambua hali halisi ilivyo Afrika na ndani ya nchi na kuona maeneo gani yana mapengo na yapi ya kusaidiwa.

"Tunataka kusaidiwa hadi wapi ili twende kuyawasilisha duniani na kuona kuikuza Afrika eneo la haki za wanawake kiuchumi, nahimiza jamii nzima kuachana na mtazamo hasi kwa wanawake, si viumbe dhaifu ni imara na wenye nguvu kama wanawake wengine,"alisema.

"Tuna nguvu za kisaikolojia, tunabeba mambo mengi kwenye akili zetu. Pia mioyo na vifua vyetu, tunastahimili mengi, tunanguvu kwenye matumbo, tunabeba viumbe na kuleta duniani, ni nguvu ambayo tumependelewa wanawake wanaume hawakupewa nguvu hiyo," aliongeza.

Alisema mwanamke ni nguzo ya maendeleo wajitambue, wajizatiti na kutekeleza wajibu wao.

"Wanawake ni chachu ya maendeleo katika taifa na hakuna taifa linaloendelea bila kuwategemea wanawake na kwasababu kubwa mbili wanawake ni wengi kuliko wanaume, wanawake ndio wanaolea dunia ndio iliyoleta wanadamu duniani."

"Wanawake ni taifa kubwa hatutakiwi kuwa wanyonge ni ukweli wanawake wanatoa mchango mkubwa kwenye shughuli za maendeleo na harakati za kukomboa taifa letu,"alisema.

"Tuna udhaifu lakini tusiubebe kama udhaifu tubebe kama kivutio kuvuta wengine kutusaidia, tunaweza kufanya, huko nyuma hatukudhani kwamba tuna weza kuwa na Rais mwanamke na afanye, lakini kwa kuwa nipo kwenye maji ya moto nafanya, nasema hivi kwasababu kuna jukumu la 50 kwa 50 kuna mambo tusipofanya vizuri hatutafika huko."

"Mbele yetu kuna mambo mengi ya kufanya tunataka wanawake tuwapo huko tusipokoleza rangi hatutaaminiwa na kufikia kwa hiyo tukoleze rangi sasa hivi tupo kwenye kiti ili tuaminiwe zaidi, kila mmoja ni super woman tuende tukaruke tukaoneshe,"alisema.

Rais alisema jitihada kubwa zimefanyika katika kuwawezesha kiuchumi wanawake ambapo imeanzishwa mifuko 61, kuna kazi ya kufanyika ya kuangalia uhai wa mifuko hiyo.

**BENKI YA WANAWAKE**

Kuhusu benki ya wanawake, alisema haikufanya faida na haikutoa mikopo kwa wengi na kusababisha kuunganishwa na benki nyingine ambayo ni benki ya posta.

"Sasa tutakapofanya vizuri kuna uwezekano wa kurudisha benki ya wanawake, tusipofanya vizuri tukaendelea kusuasua tutaendelea kubaki benki ya posta,"alisema.

**MAJUKWAA YA UWEZESHAJI**

Samia alisema kwa sasa anajipanga kikamilifu kuyalea majukwaa ya uwezeshaji wanawake kiuchumi aliyoyaanzisha wakati akiwa Makamu wa Rais.

Alisema majukwaa 23 yaliundwa ambapo 18 na majukwaa 144 ngazi ya wilaya, 302 kata na 522 ngazi ya kijiji yapo yanaendelea kufanya kazi.

"Niagize mikoa na halmashauri kuendelea kuyatunza majukwa haya, nalisisitiza hilo kwasababu sasa hivi najipanga kikamilifu kuyalea majukwaa haya,"alisema.

## HABARI KITAIFA



Balozi wa Namibia nchini Tanzania, Lebbius Tangeni Tobias, akipokea makabrasha yanayohusu mahakama kutoka kwa Rais wa Mahakama ya Afrika, Jaji Imani Aboud, jijini Arusha. Balozi huyo alifanya mazungumzo na Jaji Imani yaliyogusa nchi hizo mbili. Balozi Tobias aliihakikishia mahakama hiyo ushirikiano wa taratibu za kuanzisha mahakama ya umoja wa kiafrika. **PICHA: MAHAKA YA AFRIKA**

# Makala kuanza na haya Dar

**Na Maulid Mmbaga**

MKUU wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makala, amebainisha mikakati mitano anayoifanya na anayotarajia kuifanya katika mkoa huo.

Katika kikao na uongozi wa Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni jana, Makala alisema anaandaa mkakati wa kutembea maeneo mbalimbali ili kugagua miradi ya maendeleo na kuona namna viongozi wanavyotimiza wajibu wao katika kutatua kero za wananchi.

Alisema katika mikoa yote mitatu alikopita; Kilimanjaro, Katavi na Mbeya akiwa Mkuu wa Mkoa, utaratibu wake ni kushirikiana na viongozi wote katika kutatua kero za wananchi.

Alisema kazi ya kwanza katika Mkoa wa Dar es Salaam ni kuhakikisha anaongoza kuwa na amani na utulivu kwa kuwa huo ndiyo msingi wa watu kufanya shughuli za maendeleo, hivyo ajenda ya kupambana na uhalifu iwe endelevu.

Makala aliagiza kamati zote za ulinzi na usalama kuanza kufanya kazi kwa kushirikiana ili kuhakikisha ujambazi na uhalifu wote wanaukomesha ndani ya mkoa huo ili kuondoa malalamiko kwa wananchi.

"Kuna vijana wanafanya uhalifu halafu tunapishana nao mitaani, anasema mimi nikiingia pale sikai sana ninatoka.

"Nimeshaletewa malalamiko ya wananchi kuhusiana na hayo na nimetoa maagizo kwa utawala kuwa waanze na wakuu wa vituo ambao wanalalamikiwa ili kujenga imani kwa Jeshi la Polisi, haki itendeke," alisema.

Alisema jambo lingine ni usafi, akibainisha kuwa mwanzoni mwa wiki, alikutana na maofisa afya na mazingira na akawaeleza azma yake kwamba usafi katika mkoa huo uwe endelevu.

Alisema kipaumbele cha tatu ni usimamiaji wa miradi ya maendeleo, akiagiza viongozi kusimamia miradi yote ndani ya mkoa huo ili ifanyike kama ilivyopangwa kwa niaba ya wananchi.

Alisema mkoa huo una fursa nyingi za maendeleo, akitolea mfano eneo la fukwe na kuagiza viongozi wawe ubunifu wa vitu vitakavyoingizia serikali mapato.

Makala alisema eneo la nne analolipa kipaumbele ni udhibiti wa mapato, akiagiza madiwani kuhakikisha wanadhibiti vizuri.

# Wamiliki mashamba 89 Mvomero matumbo joto

**Na Munir Shemweta,** MVOMERO

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, ameagiza kufanyika upekuzi wa mashamba 86 yasiyoendelezwa katika wilaya ya Mvomero mkoani Morogoro.

Ameagiza kwamba yale yatakayobainika kutoendelezwa, mapendekezo ya kufutwa yapelekwe kwa Rais. Lukuvi alitoa agizo hilo jana wakati akizungumza kwa nyakati tofauti na viongozi, watendaji wa kata za wilaya ya Mvomero na wananchi wa Wami Dakawa akiwa katika ziara ya siku mbili mkoani Morogoro.

Alisema katika wilaya ya Mvomero, kuna mashamba 86 ambayo uendelezaji wake una shaka, hivyo ni vizuri ukafanyika upekuzi haraka na yale yasiyokidhi vigezo, wamiliki wapewe notisi za ufutaji na kusisitiza kuwa serikali haitaacha kuchukua hatua kwa mashamba yasiyoendelezwa.

"Ningefurahi katika kipindi Juni na Julai kazi ya upekuzi mashamba hayo iwe imefanyika ili kupunguza migogoro ya ardhi kati ya wamiliki na wananchi na lazima hatua zichukuliwe," alisema Lukuvi.

Kwa mujibu wa Lukuvi, kazi ya upekuzi mashamba ni ya msingi na waliopewa mashamba wafahamu kuwa walipewa ili kuyaendeleza na sheria inataka mmiliki walau awe ameendeleza moja ya nane ya shamba zima kwa mwaka mmoja.

"Tatizo la Mvomero ardhi imechukuliwa na wamiliki wake wamefungia hati bila kulipa kodi wala kuendelezwa na upekuzi huu unaofanyika ni kutaka kujua kila hali ya shamba" alisema Lukuvi

Naye Mbunge Mvomero, Jonas Van-zeland, alisema wilaya Mvomero ina migogoro mingi ya ardhi ikiwamo utelekezaji mashamba jambo alilolieleza kuwa limechangia wananchi kushindwa kufanya shughuli za kijamii na kuongeza kuwa wamiliki wa mashamba hayo wengi hawajulikani na wananchi.

Waziri Lukuvi katika ziara yake wilayani hapa, alisema Mvomero imekuwa na migogoro mingi ya ardhi ikiwamo ile ya mipaka ya vijiji na wilaya na kubainisha kuwa jukumu la kutafuta suluhu ya migogoro hiyo ni ya viongozi wa mkoa na wilaya.



# Hadhi Mlima Kilimanjaro kurudishwa

**Na Jenifer Gilla**

KATIKA sehemu ya pili ya makala hii tulieleza juhudi za Hifadhi ya Taifa ya Mlima Kilimanjaro (KINAPA) kurudisha hadhi ya Mlima Kilimanjaro, leo katika sehemu ya tatu na ya mwisho tunaendelea na simulizi ya juhudi hizo kutoka kwa wadau.

### KUDHIBITI VYANZO VYA MOTO

Mhifadhi Mkuu Kikoti anathibitisha kuwa wanatoa elimu kwa wasaidizi wa watalii wasiwe chanzo cha moto na pia wahakikishe wanalinda watalii.

"Tunawaelimisha kuwa walinzi wa watalii na wao wenyewe, kwamba moto unaowaka na kuthibitishwa kuwa wao au watalii waliokuwa nao ndiyo wameusababisha basi watawajibishwa ipasavyo, pia tunawakagua watalii kabla ya kuanza safari kuhakikisha kuwa hawapandi na vifaa vyovyote vinavyosababisha moto," anasema Kikoti.

Kauli inayothibitiswa na Munguatosha Mosha (32), msindikiza watalii kupitia geti la Marangu, kuwa kwa sasa majanga ya moto yamepungua kwa kazi kubwa wanayoifanya.

"Kwa sasa tunalindana wenyewe kwa wenyewe wasaidizi, ukimuona msaidizi wa mtalii yeyote anavuta sigara kiholela au kupika sehemu ambayo si husika tunamripoti, lakini hata watalii nao tunawaelimisha kuwa hawaruhusiwi kuvuta sigara njiani mpaka tufike kwenye kituo cha kupumzikia," anasema Mosha.

### KUPANDA MITI

KINAPA kwa kushirikiana na wadau wengine wa mazingira wanapanda miti katika maeneo yanayouzunguka mlima huo ili kukabiliana na joto linalosababisha theluji kupungua.

Kwa upande wao Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), linahamasisha upandaji wa miti kuanzia ngazi ya familia hadi kitaifa ili kuwa na uoto wa asili wa kutosha kusaidia kupatikana kwa hewa ya oksijeni ya kutosha ili kupunguza joto.

"Kupanda miti kwenye hifadhi pekee hakusaidii kupunguza joto, hivyo tunahitaji kuwa na miti ya kutosha katika mikoa mitatu inayozunguka mlima huu ya Kilimanjaro, Arusha, Manyara.

"Mwezi Aprili tulifanya kampeni ya kupanda miti na tulianzia hapa Arusha Aprili 1, 2021 chini ya Ofisi ya Mkuu wa Mkoa. Lengo ni kupanda miti ya kutosha ili kupunguza joto," anasema Meneja wa NEMC Kanda ya Kaskazini, Lewis Nzali.

### KUSIMAMIA MAZINGIRA

Meneja Nzali anasema pia wamekuwa wakisimamia mazingira ya kanda hiyo ya Kaskazini ili kuhakikisha kunakuwa na uoto wa asili wa kutosha kukabiliana na joto.




Mojawapo ikiwa ni kuhakikisha viwanda vikubwa vinakuwa na mfumo mzuri wa kutoa hewa ya carbon na kuhakikisha kila kiwanda kinapanda miti ya kutosha kukizunguka.

Vilevile, imekuwa ikitoa mapendekezo ya nini kifanyike ili kuilinda hifadhi hiyo wanapokutana kwenye vikao.

"Mfano tulishauri wapanda mlima wafanyiwe upekuzi kuhakikisha hawapandi na kifaa kinachosababisha moto, na tumeona yamefanyiwa kazi na kwa kiasi kikubwa kwa kuwa majanga ya moto yamepungua katika hifadhi hiyo," anasema.

Vilevile, kutokana na mamlaka walionayo NEMC imekuwa ikikagua miradi yote inayoelekezwa katika hifadhi hiyo ili kujiridhisha kama ni rafiki kwa mazingira.

Meneja huyo anatoa mfano wa mradi wa magari ya umeme (cable cars) ambao mpaka sasa haujathibitishwa kwa kuwa bado unafanyiwa thathmini kuona kama ni rafiki kwa mazingira ya hifadhi hiyo.

"Tunatumia wataalam, tunataka tujiridhishe kama kweli zile nyaya za umeme zinazotaka kupitishwa juu kama njia ya magari hayo hazitokuwa na madhara makubwa kwa hifadhi, je, ni miti mingapi itahitajika kukatwa ili njia ipatikane, tusiporidhika hautofanyika," anasema.



Ofisa Uhifadhi Mkuu anayesimamia Idara ya Sayansi na Uhifadhi katika Mamlaka ya Hifadhi ya Mlima Kilimanjaro (KINAPA), Imani Kikoti. **PICHA: MTANDAO**

### TIGO NA KAMPENI YA KUPANDA MITI

Kampuni ya simu za mkononi ya Tigo, kwa miaka sita mfululizo imekuwa ikifanya kampeni ya upandaji miti mkoani humo kupitia kampeni ya 'Tigo green for Kili' katika Wilaya ya Hai, mkoani Kilimanjaro miti hupandwa pembezoni mwa Mlima Kilimanjaro, lengo likiwa ni kurudisha theluji ya mlima huo.

Machi mwaka huu, kwa kushirikiana na taasisi ya Voice of Empowered Women Foundation ( VOEWPOFO), Tigo ilipanda miti 10,000 katika wilaya ya Hai, huku lengo likiwa ni kupanda miti 28,000 kabla ya mwisho wa mwaka.

"Tunatambua umuhimu wa Mkoa wa Kilimanjaro katika uchangiaji wa ustawi wa uchumi kwa wananchi wa mkoa huo na taifa kwa ujumla, ndiyo maana tumejikita kuilinda theluji ya Mlima Kilimanjaro ambayo ni kivutio kikubwa cha utalii nchini Tanzania, barani Afrika na ulimwenguni," alisema Mkurugenzi wa Tigo Kanda ya Kaskazini, Henry Kinabo, katika uzinduzi wa kampeni hiyo.

### MAHAKAMA YAMALIZA MCHEZO

Watu wanaokamatwa katika msitu huo hupelekwa kwenye vyombo vya sheria kwa kuzingatia Sheria ya Uhifadhi Misitu ya mwaka 2002 na nyingine zinazohusiana.

Rose Lyimo ni Mwanasheria wa kujitegemea kutoka Mahakama ya Hakimu Mkazi Moshi, anayethibitisha kupokea wahalifu watatu hadi watano kwa mwezi wanaotokana na makosa ya uvamizi wa hifadhi.

"Kesi za uvamizi wa hifadhi zimepungua ukilinganisha na miaka ya nyuma, kutokana na hukumu zilizokuwa kinatolea watu wamekuwa wanafuata sheria kwa mwezi.

"Hapa tunapokea washtakiwa wasiozidi watano kwa makosa madogo madogo, siyo yale ya kukata miti kwa biashara, yale yamekomeshwa kabisa na huwa tunawaadhibu kulingana na Sheria ya Hifadhi ya Misitu," anasema Rose.

### SHERIA YA MISITU INASEMAJE

Sheria ya Uhifadhi wa Misitu ya mwaka 2002, kifungu namba 26(a,b,s), inasema kuwa mtu yeyote haruhusiwi, kukata, kuangusha, kuchimba au kuondoa mti wowote katika eneo la hifadhi. Kuchimba au kuondoa mmea wowote wa msitu uliohifadhiwa, kuvuna, kuchukua au kuondoa mazao mengine yoyote ya msitu.

Kufanya shughuli zingine zozote ndani ya msitu wa kitaifa au wa serikali za mitaa, hifadhi ambayo ni marufuku na kanuni zinazotumika kwa msitu wote wa kitaifa, akiba au sheria zozote zinazotumika kwenye hifadhi maalum ya msitu wa kitaifa au

sheria ndogo zinazotumika kwa hifadhi maalum ya msitu ya mamlaka ya mtaa.

Wakati kifungu namba 84-5 kinasema kuwa "(5) Mtu yeyote anayetenda kosa chini ya kifungu hiki atakuwa na hatia ya kosa na baada ya kutiwa hatiani atatozwa faini isiyopungua Sh. 30,000 na isiyozidi Shilingi milioni moja au kifungo cha muda usiozidi miaka miwili au kwa faini zote mbili na kifungo.

### MAFANIKIO

Kudhibiti majanga ya moto katika hifadhi hiyo ni moja ya changamoto inayoelezwa na Mhifadhi Mkuu Kikoti, kwamba ikilinganishwa na miaka ya nyuma, kila mwaka hifadhi hiyo ilikuwa ikiungua moto sasa hali ni tofauti.

"Kwa sasa tunaweza kukaa hata miaka mitatu bila kupata kesi ya moto na hii ni kutokana na udhibiti mkubwa wa kupanda mlima na vifaa vya moto tulioufanya," anasema.

Pia elimu inayotolewa inaonekana kueleweka kwa wanakijiji hao kutokana na ushirikiano wanaoutoa kwa mamlaka ya hifadhi hiyo pale wanapoona kuna ujangili.

### CHANGAMOTO

Kila lililo jema halikosi changamoto, hali kadhalika katika harakati za kupambana na ujangili wa kukata miti kwenye hifadhi hiyo wanakutana na changamoto kadhaa ikiwamo kuzidiwa na idadi ya watu.

"Unajua hifadhi hii imezungukwa na vijiji 92 kwa hivyo 'kucontrol' (kudhibiti) wakazi wote wasivamie hifadhi ni kazi kubwa, hivyo inabidi askari wafanye kazi usiku na mchana," anasema Mkuu wa Idara ya Ulinzi na uokoaji wa KINAPA, Mapinduzi Ndesa.

# Rais Samia amlilia Mzindakaya

**Na Waandishi Wetu**

RAIS Samia Suluhu Hassan, amemwelezea mwanasiasa mkongwe, Marehemu Dk. Chrisant Mzindakaya (80), kama kiongozi mzuri, mchakapakazi na mzalendo.

Taarifa za kifo cha kiongozi huyo aliyefariki juzi katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), zilitolewa na mtoto wake, Paul Mzindakaya.

Katika ukurasa wake wa twiter, Rais Samia aliandika: “Nimepokea kwa masikitiko taarifa za kifo cha Mzee wangu, Dk. Chrisant Mzindakaya, kilichotokea leo jijini Dar es Salaam. Nitamkumbuka kwa mchango wake mkubwa katika uongozi wa nchi yetu, uzalendo na uchapakazi wake. Namwombea Mwenyezi Mungu aiweke roho yake mahali pema peponi.”

**RUKWA WAMLILIA**

Wakazi wa mkoa wa Rukwa, jana walieleza masikitiko yao juu ya kifo cha mwanasiasa huyo, huku familia ikieleza kuwa atazikwa katika eneo la makazi yake.

Akizungumza kwa njia ya simu mdogo wa marehemu, Meja Mstaafu Christopher Mzindakaya, alisema maziko yake yatafanyika eneo la Kilimani nje kidogo ya mji wa Sumbawanga.

Alisema kaka yake alikuwa akisumbuliwa na maradhi ya moyo na kwamba awali alilazwa Hospitali ya Aga Khan kabla ya kuhamishiwa MNH hadi umauti ulipomkuta.

“Familia tumeupokea msiba huu kwa masikitiko makubwa ameacha pengo kubwa kwetu alikuwa mshauri mkubwa wa familia. Mwezi mmoja uliopita akijiandaa kwenda kutibiwa, alipita hapa nyumbani kwangu, ilikuwa kama alikuja kuniaga,” alisema.

**MZINDAKAYA NI NANI?**

Dk. Mzindakaya alizaliwa Desemba 31, 1940 mkoani Rukwa. Licha ya kuwa mwanasiasa mkongwe, pia alikuwa mfanyabiashara wa mfano, mzee wa kimila na mcha Mungu.

Alijiunga na Shule ya Sekondari Bugerere nchini Uganda mwaka 1960-1961 mwaka 1963-1964, alijiunga na Chuo cha Maendeleo ya Jamii,Tengeru mkoani Arusha kwa ngazi ya cheti kisha kuwa Ofisa Maendeleo Msaidizi Wilaya ya Sumbawanga.

Alikuwa mbunge kwa miaka 45 kuanzia mwaka 1965 hadi 2010 ikiwamo mbunge wa Sumbawanga (1965- 1981), mbunge wa Kwela (1995-2010) na Mbunge kwa nafasi ya Mkuu wa Mkoa mwaka 1981 hadi 1995.

Pia alikuwa Waziri Mdogo wa Viwanda mwaka 1975 hadi 1981 na Mwenyekiti wa Bodi ya Biashara ya Ndani (BIT) mwaka 1973-1975, mwaka 1975- 1987 alikuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Shirika la Viwanda Vidogo (SIDO) 1969-175 alikuwa Mwenyekiti wa Umoja wa Vijana Tanu (TANU Youth League Mkoa wa Rukwa).

***Imeandikwa na Salome Kitomari (DAR) na Gurian Adolf (SUMBAWANGA)***

## Serikali yasitisha vibali sukari ya nje

**Na Romana Mallya,** DODOMA

WAZIRI wa Kilimo, Prof. Adolf Mkenda, amesema serikali haitatoa tena vibali vya kuagiza sukari nje ya nchi kwa wafanyabiashara kwa kuwa vina madhara makubwa kwenye uwekezaji wa viwanda vinavyozalisha bidhaa hiyo nchini.

Katika mahojiano na Nipashe jijini Dodoma jana yaliyolenga kujua hali ya sukari nchini, Waziri Mkenda alisema kwa sasa bidhaa hiyo ipo ya kujitosheleza mahitaji.

Waziri Mkenda alisema mahitaji ya ziada yalikuwa ni tani 40,000 lakini wameagiza tani 50,000 na hadi sasa zimekuja karibu zote.

“Tuna sukari ya kutosha na hakuna sababu ya bei kupanda, mtu akipandisha bei atajikuta anabaki na shehena mkononi na viwanda vingine vimeanza kuzalisha, awali vilifungwa kwa sababu ya matengenezo.

Waziri Mkenda alisema serikali itaendelea kufanya tathmini ya sukari ya ziada na mwakani endapo kutakuwa na pengo la kutaka iagizwe watakaopewa kazi hiyo ni viwanda vinavyozalisha bidhaa hiyo au Bodi ya Sukari Tanzania (SBT) na siyo wafanyabiashara kama ilivyozoeleka.

“Vibali kwa wafanyabiashara vinawavunja moyo wenye viwanda ambavyo kwa sasa vinafanyiwa upanuzi.

“Viwanda vinavyopanuliwa ni Kilombero, Mtibwa na Kagera, tunahitaji kuvilinda ili viwekeze na kuongeza uzalishaji wa sukari wa ndani,” alisema.

Prof. Mkenda alisema Tanzania haina sababu ya kutegemea sukari kutoka nje kwa sababu uzalishaji wa ndani ni mkubwa ila haujatumika kwa sababu bidhaa hiyo ilikuwa inaingia nyingi kutoka nje.

Alisema tangu serikali idhibiti uingizaji wa sukari kutoka nje kwa miaka mitano sasa, wamepunguza pengo lake kutoka tani 125,000 hadi tani 40,000 kwa mwaka.

TRA
MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA
Imethibitishwa na ISO 9001: 2015

MALIPO YA KODI KWA AWAMU NA UWASILISHAJI RITANI KWA WAKATI

Ndugu Mlipakodi, unakumbushwa kulipa kodi ya mapato ya mwaka 2021 kadri ya awamu yako pamoja na kuwasilisha ritani ya kodi ya mapato ya mwaka 2020. Aidha, kama bado hujakadiriwa kodi ya mapato kwa mwaka 2021 tafadhali fika pia TRA ukadiriwe.

Wahi sasa ili kuepuka usumbufu usio wa lazima!.

TAHADHARI: Kuwa makini na matapeli wanaotumia vibaya jina la TRA au majina ya watumishi katika kipindi hiki, hivyo jiridhishe kila wakati.

*Kumbuka: Ukiuza toa risiti. Ukinunua dai risiti*

Kwa maelezoa zaidi, piga simu bure;
0800-750075 au 0800-780078
Barua pepe: huduma@tra.go.tz WhatsApp: 0744-233-333

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Hongera serikali kuandaa wanasayansi wanawake

**SERIKALI** kuanzia mwezi ujao itaanza kujenga shule za sekondari maalumu za sayansi kwa wasichana, lengo ni kupunguza pengo kubwa kati ya wanawake na wanaume kwenye sekta ya sayansi na teknolojia.

Ni maagizo na ahadi inayotolewa na Rais Samia Suluhu Hassan, wakati akizungumza na wanawake mkoani Dodoma jana na kueleza kuwa , serikali itaanza kujenga shule moja ya sekondari katika kila mkoa yenye kufundisha masomo ya sayansi kwa ajili ya wasichana pekee.

Rais Samia anathitibisha kuwa kwa sifa zote ziwe za kutumia simu za mkononi, mitandao ya kijamii na kompyuta wanawake wako nyuma mno ikilinganishwa na wanaume na kwamba kinachofanyika sasa ni jitihada mahsusi za kuwapa nafasi wasichana kuwa sehemu ya sayansi na teknolojia ambayo ndiyo usukani unaoiongoza dunia.

Ni wazi kuwa kuendeleza wanawake kwenye sayansi kutasaidia kutatua matatizo mengi ya wanawake kwenye maeneo mengine ikiwamo nishati, maji, mazingira, afya, uchumi, elimu, uzazi na ajira. Kwa mfano , tukiangalia suala la gharama kubwa za kupata nishati ya kupikia ni dhahiri wasomi wanawake waliojikita kwenye sayansi watafanya utafiti ili kupata majibu ya changamoto za ukosefu wa nishati salama na mbadala.

Mathalani, Tanzania inabakia kwenye changamoto kubwa ya nishati ya kupikia kwa vile taifa linategemea kuni na mkaa. Licha ya kuwapo nishati kama gesi, umeme na mafuta ya taa zote hizo si rafiki kwa wanawake maana bidhaa hizo ni ghali zinahitaji kuwa na kipato kikubwa, ambacho kinamama wengi hawana. Tunaunga mkono juhudi za serikali za kujenga shule hizo kwa sababu kutoa mafunzo maalumu ya sayansi na teknolojia kwa wasichana wanaochipukia kutarahisisha utafiti unaoleta ufumbuzi wa matatizo ya wanawake kwa mfano eneo muhimu la umeme na nishati, ambalo linahitaji ufumbuzi wa haraka.

Tunaamini uwepo wa watafiti hao pengine utawezesha kubuni na kutengeneza ' gesi ya samadi 'biogas' inayopatikana kwa urahisi na kwa gharama nafuu, itakayoweza kubadili matumizi ya kuni na mkaa vijijini na kuokoa mazingira lakini pia kuziwezesha familia kupika chakula bila usumbufu.

Uwepo wa nishati hizo zinazoweza kuzalishwa kutoka kwenye mabaki ya mazao mashambani, jikoni, taka za vyooni na mbolea za mifugo tunaamini kunaweza kuondoa matumizi ya umeme ambao mara nyingi unaonekana kuwa ni wa bei kubwa na hauwezi kutumiwa kupika vyakula mijini na vijijini.

Tukiangalia zaidi suala la nishati ni wazi tangu Tanzania ilipopata uhuru miaka 60 iyopita mkaa na kuni vimebaki kuwa chanzo pekee cha kupikia iwe nyumbani, migahawani na kwenye taasisi kama elimu, magereza, vyuoni au hospitalini.

Wakati hayo yanafanyika taifa lina hazina kuu ya makaa ya mawe ambayo baadhi ya wataalamu wanasema inabidi yasafishwe kuondoa kemikali inayoungua kwa haraka na kwa nguvu zaidi ya sulphur. Kuondoa kemikali hiyo kunaaminika kuwa kunawezesha makaa hayo kutumiwa kupikia nyumbani hata hivyo ni mchakato wa gharama kubwa.


Lakini, wapo baadhi ya wenye maoni kuwa makaa ya mawe yakichanganywa na samadi au vumbi la mbao na mabaki ya mazao baada ya mavuno kama mabua yanapunguza makali ya moto wa nishati hiyo.

Hata hivyo, makaa hayo ni lazima yasafishwe na kuwa salama maana moshi wake ni hatari, hivyo tunaamini kuwa wakiwapo wanawake wanasayansi itakuwa ni fursa kubwa zaidi ya kupata majibu na kuzimaliza changamoto na matatizo yanayowakabili kinamama wa taifa hili.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

## Kero za wamachinga sokoni, barabarani zimalizike sasa

Na Sabato Kasika

**HIVI** karibuni Rais Samia Suluhu Hassan, alilizuru soko la Kariakoo jijini Dar -Es- Salaam na kuahidi kushughulikia kero za soko hilo maarufu barani Afrika, lakini akatoa neno kwa wafanyabiashara ambalo ni muhimu kulizingatia.

Rais aliwakumbusha kwa kusema; 'abebwaye hujikaza na ninyi jitahidini kufuata sheria zinazowekwa katika maeneo mlipo maana nimeona njia zote zimezingirwa, ni vibanda kila kona'.

Kauli hiyo ya Rais inawakumbusha wafanyabiashara kuwa wakati serikali inawabeba, nao wanatakiwa kufuata sheria ili kuepusha msoguano na malumbano kati yao na serikali au watu na mamalaka nyingine hasa majiji na wilaya.

Akiwa Kariakoo, Rais alishuhudia kitu alichokiita 'vurugumechi', kutokana na wafanyabiashara kufanya shughuli zao bila kuzingatia utaratibu hadi 'kuvamia kila eneo na kusababisha watu wengine kushindwa kutumia barabara.

Ufanyaji biashara wa aina hiyo haupo Kariakoo tu, bali karibu maeneo yote ya masoko ya Tanzania kuanzia jijini Dar es Salaam hadi Makoroboi Mwanza mpaka Mwanjelwa Mbeya hali ambayo inaonyesha wazi kwamba kuna haja viongozi wa hamashauri kuwaweka kwenye maeneo rasmi ya biashara.

Kwa sasa wapo wanaopanga biashara kwenye vituo vya daladala na kusababisha usumbufu kwa madereva na abiria, kwa kuwa wakati mwingine magari yanakosa sehemu ya kupita kwa sababu yao.

Wengine wanapanga bidhaa kwenye barabara zinazoendelea kujengwa, huku mama na babalishe, wachoma mahindi, viazi na wakaanga chipsi na ndizi kwa upande wao, wanawasha moto kwenye vituo vya mabasi na popote penye upenyo.

Hivyo ndivyo ilivyo kwenye baadhi ya vituo vya daladala, mabasi na kwenye njia za wanotembea, madaraja, juu ya mitaro ni kama wanaozimiliki wao hali inayosababisha usumbufu kwa watumiaji.

Kwa mazingira hayo ni kama 'vurugumechi' aliyosema Rais Samia alipotembelea soko la Kariakoo, kwani kinachoendelea sasa ni kama wamejimilikisha baadhi ya barabara.

Ikitokea bahati mbaya mpita njia akakanyaga bidhaa za mmachinga, anaweza kujikuta katika wakati mgumu kwa kutukanwa matusi ya nguoni, kana kwamba hana haki ya kutumia njia au barabara.

Njia bora itakayoondoa mkanganyiko huo, ni kuwapeleka katika masoko yao kama yapo, au kutenga maeneo rasmi kwa ajili ya usalama wao na wa watu wengine ambao ni watumiaji wa barabara na vituo vya daladala.

Vilevile jiji la Dar- es- Salaam linaweza kuweka utaratibu bora ambao makundi yote hayo yatanufaika nao na ikibidi, itengwe hata mitaa maalum kwa ajili yao, ambayo haiingiliani na shughuli nyingine.

Kuendelea kufanya biashara katika mazingira ya sasa ni sawa na vurugumechi au 'mchafukoge' ambazo zinaweza kusababisha watu wakaumizana au wakaungua kwa moto wa kupikia vyakula unaowashwa vituoni.

Kwa mfano, abiria ni wengi kituoni, usafiri ni wa shida, halafu inakuja daladala wanaanza kukimbizana kuwawahi kupanda na bahati mbaya mmoja wao akajigonga kwenye jiko lenye maji yanayochemka. Hilo linaweza kusababisha ajali watu wakaungua, hivyo umuhimu wa kuepusha abiria na wafanyabiashara wenyewe katika hatari, ni kila upande kuwa na eneo lake, kuliko kujichanganya pamoja huku wengine wakifanyabiashara hatarishi.

Itapendeza iwapo vituo vya daladala vitabaki kuwa vya abiria na maeneo ya kupika na kuuza vyakula yake kwa ajili ya mama lishe, baba lishe na wengine wanaojishughulisha na biashara hiyo.

Lakini pia, itapendeza iwapo barabara zitaachwa kwa ajili ya magari na zile za waenda kwa miguu zikabaki kwa ajili yao, kuliko kuvamiwa na wamachinga na kuzigeuza kuwa eneo la biashara tena zinazotandazwa chini na kusababisha usumbufu kwa wengine na uchafu wa mazingira na vyakula.

TANGAZO

MeTL GROUP The People's Brand

Juhudi Za
KUBORESHA MAISHA YA WATANZANIA

mo ASSURANCE Mo Coverage, More Peace

# MeTL wauzaji wa pikipiki na bajaj wanaoongoza nchini

Na Mwandishi Wetu

Sekta ya usafirishaji hususan wa pikipiki za boxer na 3-wheelers maarufu bajaj imeajiri idadi kubwa ya Watanzania. Na kwa kiasi kikubwa maisha yao yameendelea kuboreshwa kila uchwao na kuondokana na utegemezi wa ajira.

Ili vijana wengi waweze kupiga hatua unahitaji vyombo hivi viweze kudumu kwa muda mrefu ili viendelee kuwanufaisha wao ili watimize malengo yao kwa wakati.

Mahali pa kupata bajaj na pikipiki bora ni sehemu moja tu pekee, M/s Mohammed Enterprises (Tanzania) Ltd.

MeTL ni wauzaji na wasambazaji wakuu nchini waliothibitishwa na kampuni ya Bajaj Auto Ltd kwa pikipiki za boxer na bajaj.

Kampuni ya Bajaj Auto Ltd inauza bidhaa nyingi ikiwamo pikipiki za boxer za 100 mpaka 150 cc, pulsar, discover, dominor za 400 cc na 3 wheelers, Bajaj RE 250, Maxima Cargo and 4-wheeler intra city smart cab - Qute kwa Tanzania.




Jengo la ofisi ya Kampuni ya Mohamed Enterprises Limited (MeTL) inayouza bajaj na pikipiki.

Bajaj Auto Ltd ni kiongozi wa soko duniani kwa kuuza vyombo vya moto vinavyofanya shughuli zake ndani ya miji. Ni nembo ya kibiashara inayofahamika vyema kwa kuzingatia ubora, mwendokasi, unyumbulifu na ndiyo kampuni ya kwanza kufanya biashara ya vyombo vya moto vya magurudumu matatu (Bajaj) kwa Tanzania ambavyo vinapendwa na mamilioni ya watu.

Kampuni hiyo inatajwa kuwa ni mzalishaji mkubwa wa tatu (3) wa pikipiki na wa kwanza wa bajaj duniani kwa sasa. Inashika nafasi ya 96 katika orodha ya kampuni 100 vumbuzi ya jarida mashuhuri la Forbes la Marekani mwaka 2014.

Kampuni hiyo inauza bidhaa zake kwa zaidi ya nchi 70 ulimwenguni na mauzo yake ya pikipiki takriban milioni 5 yanakwenda katika kila pembe ya dunia.

Muuzaji huyo wa Bajaj, anamiliki kiwanda cha kuzalisha vyombo hivyo kwa Afrika Mashariki na Tanzania. Kiwanda hiki kina uwezo wa kuzalisha pikipiki 200 kwa awamu. Bidhaa ya pikipiki za boxer ndiyo inayoongoza kwa mauzo kwa Tanzania na Afrika kwa ujumla. Kampuni hiyo inapatikana katika miji 25 na ina washirika 177 kote nchini.

# MO Assuarance inavyotoa huduma bora za bima kwa kila Mtanzania




Donati Mbobezi (kushoto) akipokea fidia ya madai ya upotevu wa mifugo yake kwa hundi yenye thamani ya Sh 1 Milioni na 200,000 kutoka kwa moja ya wafanyakazi wa Kampuni ya Bima ya Mo kupitia Timu ya Dhamana.

Maliki Muunguja, Mwananchi

Kwa kawaida watu wamekuwa wakidhani kuwa kukata bima ni kupoteza fedha, lakini ukweli haupo hivyo, bima inakusaidia kukukinga wewe, familia na mali zako dhidi ya matukio tusiyoyatarajia.

Matukio kama ajali, ugonjwa na kifo huweza kumkuta mtu mara nyingi akiwa hajajiandaa hivyo bima hukusaidia kukuepusha na adha ya kukosa fedha kwa ajili ya kushughulikia mambo yanapojitokeza. Jambo la msingi ni kwamba unahitaji mtoa huduma za bima atakayekushika mkono, na kwa mantiki hiyo, kampuni ya Bima ya Mo imesikia vilio vya Watanzania wengi wenye vipato vya chini vya kutaka bima inayoendana na hali zao.

Kampuni ya Bima ya Mo (Mo Assurance Company Limited) ilianza kuendesha shughuli zake Machi 1, 2007 na imejiimarisha kama mtoa huduma za bima thabiti na anayekua sokoni akichagizwa na mchanganyiko wa bidhaa zenye tija sambamba utoaji wa huduma ndogo za bima.

Ikumbukwe kuwa, kabla ya MO Assurance, kampuni hii ilijulikana kama Golden Crescent Assurance ikiingia katika sekta ya fedha kwa ufadhili wa Kundi la m-akampuni ya METL (Mohamed Enterprises Tanzania Limited).

Kampuni inatoa bima zisizo za maisha ikiwa ni pamoja na bima ya matibabu, safari, magari, moto, uhandisi, bahari, hati fungani na bidhaa zinginezo. Mauzo ya bima ya kampuni hiyo yamekua kwa kiasi kikubwa kutoka kiasi cha Sh8 bilioni mwaka 2018 hadi Sh18 bilioni mwaka 2020.

Kampuni hiyo inayomilikiwa na Watanzania kwa asilimia 100, ina matawi Arusha na Mwanza na hivi karibuni watafungua tawi huko Zanzibar. Pia, kampuni hiyo inatoa rufaa katika hospitali za nje ya nchi kwa wateja wa bima ya afya pale inapolazimu.

MO Assurance ni miongoni mwa kampuni za kwanza kutambulisha bima ya simu ya mkononi kupitia mipango yao ya huduma ndogo za bima ya maisha na afya. Chini ya mwamvuli wa huduma ndogo za bima za kampuni hiyo, zaidi ya wateja 600,000 wamekatiwa bima.

### Kwa nini nichague MO Assurance?

Kampuni hii inawajali wateja wake kwa kuwapa kipaumbele katika kila jambo.

Pia, kampuni inashughulikia madai ya wateja kwa misingi ya haki, usawa na haraka.

Kampuni imeajiri watu wenye weledi na uzoefu kuelewa mahitaji yako ya bima, wanatoa tathmini ya haraka na ushauri, na ulinzi wa kutosha wa bima kwa bei shindani zaidi.

Sifa nyingine ni kuwa kampuni hii ina nguvu ya kifedha na pia inafadhiliwa na watoa huduma za bima wengine walio na nguvu ya kifedha.

### Huduma kwa wateja

Kampuni inafahamika kwa wateja wake kama mtoa huduma bora za bima na uzoefu wa aina yake. Imejitolea kuwapa wateja wake huduma nzuri, rafiki na shindani. Pia, kampuni hiyo ina huduma za mawasiliano kwa wateja wake kupitia simu ya dharura ambayo inafanya kazi masaa 24. Muda wote wako tayari kuwasikiliza wateja wake kwa jambo lolote lile kupitia namba: +255 745 600 100.

### Dira ya kampuni

Kampuni inatazamia kuwa mtoa huduma za bima anayependelewa zaidi na Watanzania.

Mdau anayewajibika, mwenye weledi, mwadilifu na mpenda usawa katika shughuli zake na anayefuata kanuni za utawala bora na uwajibikaji kwa jamii.

### Matarajio

Inataka kuhakikisha kuwa kampuni ya Bima ya Mo inabaki kuwa shindani kwa siku zijazo na kuchangia usalama wa kifedha wa wateja na wafanyakazi wake.

## TANGAZO


METL GROUP The People's Brand
Juhudi Za
KUBORESHA MAISHA YA WATANZANIA
mo ASSURANCE
MO ...tunagusa maisha yako.
BAJAJ
LOVED IN 70 COUNTRIES
VUTA CHOMBO UJIPATIE
BIMA
BURE
NUNUA BAJAJ AU BOXER
UPATE BIMA NDOGO BURE KUTOKA
MO ASSURANCE
T&C APPLY
mo ASSURANCE
Mo Coverage, More Peace
TOLL FREE: 0800 710 060
WASILIANA NASI: +255 22 2127398 | +255 22 2129981

HABARI KITAIFA

# CHADEMA, CUF vyatulizwa kutosusia uchaguzi mkuu 2025

**Na Sabato Kasika**

VYAMA vya CUF na CHADEMA, ambavyo vimetangaza kususia uchaguzi mkuu wa mwaka 2025, hadi ipatikane katiba mpya, vimetakiwa kuachana na msimamo huo, kwa madai kwamba unaweza kusababisha vikayumba.

Badala ya kususia uchaguzi, vimetakiwa kukaa katika meza ya mazungumzo kwa kuwa ndiyo inaweza kuleta mwafaka kwenye suala la katiba mpya kuliko hatua zilizotangazwa na viongozi wa vyama hivyo.

Wito huo ulitolewa na Mwenyekiti wa Taasisi ya Utawala Bora na Maendeleo Tanzania (CEGODETA), Thomas Ngawaiya, kwa kusema katiba ni muhimu kwa manufaa ya Watanzania wote, lakini pia si vizuri vyama kususia uchaguzi.

"Ushauri wetu kama wadau wa utawala bora, ni kwamba vyama hivyo, viitishe meza ya mazungumzo na pia kushawishi Watanzania wengi zaidi kujua umuhimu wa wa katiba mpya, siyo kususa," alisema Ngawaiya.

Alisema, nchi hii ni ya vyama vingi, hivyo CUF na CHADEMA vikisusa, vingine vinaweza kushiriki na kujizolea madiwani na wabunge na kuvifanya vilivyosusa viyumbe na hatimaye kukosa nguvu za kushawishi Watanzania.

"Kama unafuatilia siasa za Tanzania, utagundua kuwa kila mwaka wa uchaguzi zimekuwa vikijitokeza vyama ambavyo havitarajiwi na kushiriki kuanzia kampeni hadi uchaguzi," alisema.

Alisema, mazingira kama hayo ndiyo yanaweza kuvikumba vyama ambavyo vimetangaza kususia uchaguzi, na kwamba viongozi hao wasitarajie kuwa wanaweza kuungwa mkono na wenzao wa vyama vingine.

"Hata hivyo, kwenye suala hili la katiba mpya, Rais Samia Suluhu Hassan ameshaomba apewe muda, hivyo ni vyema kauli hiyo ikaheshimiwa, kwani ana muda mfupi tangu ashike usukani," alisema.

Novemba mwaka jana, Mwenyekiti wa CUF, Prof Ibrahim Lipumba, alitangaza kuwa chama hicho haitashiriki uchaguzi wowote badala yake kitajikita katika harakati za kudai katiba ili tume huru ya uchaguzi ipatikane.

Hivi karibuni, Mwenyekiti wa CHADEMA, Freeman Mbowe, naye alitangaza uamuzi kama huo wakati uzinduzi wa oparesheni ya iitwayo 'Haki', yenye lengo la kusajili wanachama wapya kidigitali kote nchini.



Mkurugenzi Mtendaji wa Tigo Tanzania, Simon Karikari akipanda mti kuadhimisha Siku ya Mazingira Duniani katika Wilaya ya Hai, mkoani Kilimanjaro mwishoni mwa wiki, ikiwa ni sehemu ya kampeni ya Tigo Green for Kili ya kuhifadhi mazingira ya Mlima Kilimanjaro. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Ofisa mipango kortini kwa tuhuma za rushwa

**Na Said Hamdani,** LINDI

OFISA Mipango wa Halmashauri ya Wilaya ya Nachingwea, mkoani Lindi, Ally Nnunduma Abdallah (48), amepandishwa katika Mahakama ya Wilaya, akituhumiwa kujihusisha na vitendo vya rushwa ya Sh. milioni 4.6.

Imedaiwa kuwa alipokea fedha hizo kutoka kwa mmoja wa wafanyabiashara kwa lengo la kumdhulumu mwajiri wake.

Mtuhumiwa huyo alifikishwa mbele ya Hakimu Sikitu Mwalu Samba na kusomewa shtaka na Mwanasheria wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Lindi, Osborn Mulamula.

Mulamula akisoma shitaka hilo alidai mtuhumiwa alihaidi hongo kwa mmoja wa wafanyabiashara wa mjini Nachingwea ili ampatie risiti ya elektroniki (EFD) yenye thamani ya Sh. 4, 625,000, ikionyesha ametekeleza ununuzi wa vifaa vinavyohitajika.

Pia, alidai lengo la mtumishi huyo kufanya hivyo ni kutaka risiti hiyo aipeleke kwa mwajiri wake kwa lengo la kumdanganya kuwa ametekeleza kile alichokiombea kununua vifaa husika.

Mulamula alidai kwamba mtuhumiwa aliomba kiasi hicho cha fedha kutoka kwa mwajiri wake Halmashauri ya Wilaya ya Nachingwea, kununua vifaa ambavyo hata hivyo, havikutajwa, badala yake alizitumia kwa manufaa yake binafsi.

Hata hivyo, mshtakiwa ambaye yupo nje kwa dhamana, alikana kosa na kesi hiyo namba 53/2021 imepangwa kwa usikilizaji wa awali Juni 23, mwaka huu.

# Wadau wa mazingira wasafisha Coco Beach

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI saba waasisi wa PETCO Tanzania, kwa kushirikiana na wadau wengine wa mazingira, wameshiriki kusafisha fukwe ya Coco-Beach jijini Dar es Salaam na kutoa elimu kuhusu taka za chupa za plastiki.

Akizungumza katika hafla hio, Mkurugenzi wa Mahusiano ya Jamii, Mawasiliano ya Umma na Ukuaji Endelevu wa Coca-Cola Kwanza, Salum Nassor, alisema lengo kuu la PETCO Tanzania ni kuwezesha ukusanyaji na uchakataji wa chupa za plastiki baada ya matumizi.

Kadhalika, alizipongeza kampuni zingine waasisi kwa kuweka upinzani wa kibiashara kando na kuungana katika jambo hilo linalogusa mazingira na Watanzania.

Nassor alitoa wito kwa kampuni zingine kutoka sekta tofauti kuiga mfano huo na kuwaalika kwenye biashara ya chupa za plastiki kujiunga PETCO Tanzania.

Mkurugenzi wa Mahusiano ya Jamii wa SBC Tanzania (Pepsi), Foti Gwebe, alisema wanajivunia kuwa miongoni mwa waanzalishi wa PETCO kwa sababu wanaamini itasaidia kupunguza taka za plastiki na pia kuongeza ajira nchini.

Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Exaud Kigahe, alisema amepata faraja kuona kampuni hizo zikikaa pamoja kwa ajili ya mambo ya mazingira na kijamii.

Kigahe alisema: "Huu ni mfano wa kuigwa na Serikali iko pamoja na wamiliki wa viwanda kuhakikisha wanaendeleza gurudumu la maendeleo mbele lakini pia kuhakikisha wanaacha mazingira katika hali salama."

Waasisi wa PETCO Tanzania ni Coca-Cola Kwanza, Pepsi Tanzania, SILAFRICA Ltd, A-One, Sayona na Nyanza Bottlers.

# Wakulima pamba, tumbaku kulipiwa Bima ya Taifa Afya

**Na Shaban Njia,**KAHAMA

CHAMA Kikuu cha Ushirika Kahama (KACU), kimesema kimejipanga kuwalipia gharama za kujiunga na Bima ya Taifa ya Afya (NHIF) wakulima wake wa tumbaku na pamba 7,390 yenye thamani ya Sh. milion 913 baada ya kununua na kuuza pamba kilo milioni 10 msimu huu.

Wakulima hao ni kutoka Halmashauri za Ushetu, Msalala na Manispaa ya Kahama, huku wakulima wa pamba wakiwa 6,800 na tumbaku wakiwa 590 na wote watapa bima hizo bila kujali kiwango cha uzalishaji wa mazao hayo.

Mwenyekiti wa KACU, Emmanuel Charahani, aliyabainisha hayo jana wakati wa utiaji saini makubaliano ya bima ya afya kwa wakulima baina ya benki ya cRDB, NHIF na KACU.

Alisema kuwa,msimu huu wanatarajia kununua pamba kilo milioni 10 ,faidi ya malipo ya pili yatayopatikana kwa asilimia 100, na kwamba atahakikisha anapunguza Sh.50 na kuwalipia wakulima bima ya afya ili kuondoa makato watayokatwa na benki baada ya kuuza mazao yao.

# Ukaguzi kufanywa mikopo wanawake, vijana

OFISI ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), imesema itafanya ukaguzi kuangalia utoaji na urejeshaji wa mikopo inayotolewa kwa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu.

Naibu Waziri wa Ofisi hiyo, Dk. Festo Dugange, aliyasema hayo bungeni jana alipokuwa akijibu swali la nyongeza la Mbunge wa Maswa Mashariki (CCM), Stanslaus Nyongo. Katika swali lake, Nyongo alisema fedha za mikopo zimekuwa zikitolewa na halmashauri lakini hawaoni namna gani zinavyorudishwa ili wakopeshwe watu wengine.

Kutokana na hali hiyo, alihoji serikali ina mpango gani kuweka mkakati thabiti wa kuhakikisha fedha zinaporudi wanapewa watu wengine ili kujiendeleza kibiashara.

Akijibu swali hilo, Dk. Dugange aliwataka wakurugenzi wa mamlaka za serikali za mitaa kusimamia mikopo na marejesho ili fedha hizo zirudi na kuwanufaisha wengine.

"Ni kweli fedha hizo zimekuwa zinatolewa kwa vikundi vya wajasiriamali katika mamlaka za serikali za mitaa kupitia mapato ya ndani ya asilimia 10. Kwa mujibu wa sheria na kanuni, zinatakiwa kuzunguka na kila kikundi kinachokopeshwa kinapaswa kurejesha bila riba ili wakopeshwe wengine," alisema.

Hata hivyo, alisema kumekuwa na tatizo la urejeshwaji wa fedha hizo kwa baadhi ya vikundi vinavyokopeshwa na sheria sasa imeweka utaratibu mzuri wa kuhakikisha wanafungua akaunti maalum ili kurejesha fedha hizo.

"Nichukue nafasi hii kuwaelekeza wakurugenzi wa mamlaka za serikali za mitaa kuhakikisha wanalisimamia kwa karibu sana suala la mikopo na marejesho. Sisi TAMISEMI tutakwenda kufanya ukaguzi kuona fedha zilizokopeshwa zinarejeshwa na zinaendelea kukopeshwa katika vikundi vingine,"alisema.

Katika swali la msingi, Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Mwantumu Dau Haji, alihoji ni lini serikali itaanza kutoa elimu ya ujasiriamali kwa wanawake na vijana katika kalmashauri wanaopewa mikopo ya asilimia tano. Naibu Waziri alisema kwa mujibu wa Kanuni ya 23 ya Kanuni za Utoaji na Usimamizi wa Mikopo ya asimilia 10 kwa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu za mwaka 2019, mamlaka za serikali za mitaa zinapaswa kutoa mafunzo kwa vikundi vilivyokubaliwa kupata mikopo hiyo.

Alifafanua kuwa kwa kuzingatia kanuni hiyo, serikali ilikwishaanza kutoa elimu ya ujasiriamali na katika mwaka wa fedha 2019/20.

"Mamlaka za serikali za mitaa zimetoa mafunzo kwa vikundi 11,915 vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu ambavyo vilipewa mikopo inayotokana na asilimia 10 ya mapato ya ndani ya halmashauri zote nchini," alisema.

Alisema mafunzo yaliyotolewa ni pamoja na ujasiriamali, utunzaji fedha, uendeshaji na usimamizi wa miradi, utoaji taarifa na usimamizi wa marejesho ya mikopo.

"Serikali kupitia mamlaka za serikali za mitaa itaendelea kutoa elimu kwa vikundi hivyo ili kuvijengea uwezo wa kuendelea kukua na kutumia ipasavyo fursa mbalimbali za kiuchumi katika maeneo yao,"alisema.



Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, akizungumza na wabunge, Edward Ole Lekaita (Kiteto) na Anne Kilango Malecela (Same Mashariki), Bungeni jijini Dodoma juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Uwanja ndege Singida wafanyiwa upembuzi yakinifu ufadhili wa WB

WIZARA ya Ujenzi na Uchukuzi imesema kiwanja cha ndege cha Singida ni miongoni mwa viwanja 11 vilivyofanyiwa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ufadhili wa Benki ya Dunia kupitia mradi wa TSSP.

Naibu Waziri wa wizara hiyo, Mwita Waitara, alisema jana bungeni alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Singida Magharibi (CCM), Elibariki Kingu.

Kingu alihoji ni lini serikali itaanza ujenzi wa uwanja wa ndege wa Singida ili ndege za Shirika la Ndege Tanzania (ATCL) zianze kutua na kurahisisha usafiri.

Akijibu swali hilo, Waitara alitaja viwanja vingine kuwa ni Lake Manyara, Musoma, Songea, Kilwa Masoko, Tanga, Iringa, Lindi, Moshi, Singida Njombe na Simiyu.

Alisema baada ya hatua ya awali ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kukamilika, serikali imejipanga kuanza hatua ya ujenzi kwa viwanja vyote kwa awamu kwa kutumia fedha za ndani kutokana na gharama za ujenzi wa viwanja hivyo kuwa kubwa ukilinganisha na bajeti inayotengwa kila mwaka.

Waitara alibainisha kuwa kwa kuzingatia bajeti, serikali kupitia Wakala wa Barabara nchini (TANROADS) imejipanga kuanza na ujenzi wa viwanja vya Iringa na Songea. "Ujenzi wa viwanja vilivyobaki kikiwamo cha Singida, utaanza mara serikali itakapopata fedha. Kwa sasa serikali inaendelea kuwasiliana na washirika wa maendeleo ili kupata fedha za kujenga viwanja hivyo," alisema.

Alimwomba mbunge huyo na wananchi wa Singida waendelee kuvuta subira kwa kuwa serikali ina nia ya dhati ya kujenga kiwanja hicho.




Habari zote na Augusta Njoji

## Ajira walimu zachambuliwa

SERIKALI inachambua maombi ya ajira 6,949 za walimu za shule za msingi na sekondari zilizotangazwa mwezi uliopita, bunge lilielezwa jana mjini hapa.

Naibu Waziri Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Dk. Festo Dugange, alisema alipokuwa akijibu swali la nyongeza la Mbunge wa Mlalo (CCM), Rashid Shangazi.

Katika swali lake, Mbunge huyo alisema kwa sasa serikali iko kwenye mchakato wa zaidi ya ajira 6000 na upungufu ulioko Lushoto ni wa zaidi ya walimu 1,000.

"Je, serikali haioni umuhimu wa kuipa Halmashauri hiyo kipaumbele katika ajira hizo?" alihoji.

Pia alisema kwa kuwa wako walimu ambao wanataka kurudi Lushoto kutoa huduma ya elimu lakini changamoto ni uhamisho, hivyo kuhoji kama serikali iko tayari kuungana naye kuwabaini ili kuondoa uhaba huu wa walimu Lushoto.

Akijibu swali hilo, Dk. Dugange alisema katika ajira hizo serikali itatoa pia kipaumbele kwa Lushoto.

Alikiri kuwapo kwa upungufu wa walimu lakini serikali imeendelea kuajiri kwa awamu na katika ajira hizo zaidi ya 6,000 ambazo tayari hatua za kuwapata zinaendelea.

"Kwa wanaotaka kurudi kufanya kazi katika halmashauri hiyo utaratibu upo na unaruhusiwa lakini kwa wenye sababu za msingi hivyo wafuate taratibu za kuomba uhamisho kwakuwa serikali ipo tayari kuwapa kibali kama wana vigezo,"alisema.

Katika swali la msingi, Mbunge huyo alihoji serikali ina mpango gani kupeleka walimu katika halmashauri hiyo.

Shangazi alisema halmashauri hiyo ina upungufu wa walimu wa shule za msingi takribani 1,270 na kuhoji, serikali ina mpango gani wa kupeleka walimu katika Halmashauri hiyo.

Akijibu swali hilo, Dk. Dugange alisema katika kipindi cha kuanzia mwaka wa fedha 2016/17 hadi 2019/20 serikali imeajiri na kuwapanga walimu 148 wa shule za msingi na walimu 118 wa shule za sekondari katika Halmashauri hiyo.

Alifafanua idadi hiyo kati ya walimu 26,181 wa shule za msingi na sekondari walioajiriwa katika kipindi hicho.

Aidha, alisema serikali inaendelea kuratibu kazi ya kuajiri walimu 6,949 kwa nafasi za ajira zilizotangazwa mwezi Mei 2021 ambao watapangwa kwenye shule mbalimbali zikiwamo za Wilaya ya Lushoto.

## Mkataba AfCFTA ndivyo taifa litakavyonufaika

Ukurasa 13



Ukurasa 14




siasa

JUMATANO JUNI 9, 2021

Nipashe

HABARI BORA NA KAMILIFU

# Katiba ni hitaji la taifa si la upinzani

## ■ Uchaguzi chama kimoja ni hasara

**Na Sabato Kasika**

BAADA ya CHADEMA na CUF kutishia kususia uchaguzi mkuu wa 2025 iwapo hakutakuwa na katiba mpya na tume huru ya uchaguzi, watalaamu wa siasa na masuala ya sheria wameitumia salamu serikali kuwa, katiba mpya haina mbadala.

Wadau hao wanasema kuwa katiba iliyopo imeshapitwa na wakati, haiendani na mahitaji ya zama zilizopo, na kwamba suala la kuandikwa katiba mpya halikwepeki, hivyo linatakiwa kufanyiwa kazi na si kwa sababu ya uamuzi wa CHADEMA na CUF.

Kadhalika wanavikumbusha vyama hivyo kuwa visiposhiriki katika uchaguzi, ni hasara kwa demokrasia na kwamba, kama nchi, itakuwa imepoteza kile ambacho dunia inakisisitiza nacho ni demokrasia.

### WATANZANIA WANAIHITAJI

Kutokana na msimamo wa vyama hivyo kususa uchaguzi wa 2025, Nipashe inazungumza na baadhi ya wachambuzi na wadau wa siasa kupata maoni yao jinsi wanavyouchukulia iwapo serikali itachukua hatua za kuleta katiba mpya au kunyamaza.

Mchambuzi wa siasa ambaye pia ni Mjumbe wa Bodi ya Jukwaa la Katiba Tanzania (JUKATA), Hebron Mwakagenda, anasema katiba mpya ni hitaji la Watanzania wote wakiwamo wanachama wa CCM.

Anasema, katiba iliyopo imeshapitwa na wakati, haiendani na mahitaji ya wakati sasa, na kwamba suala la kuwapo kwa katiba mpya halikwepeki, hivyo linatakiwa kufanyiwa kazi.

"Najua Rais Samia Suluhu Hassan alishaomba kwamba apewe muda kidogo, lakini mimi ninashauri ashughulikie jambo hili mapema lingali la moto asije kukutana na wajanja wakamshawishi kinyume," anasema Mwakagenda.

Anaeleza kuwa anafahamu kuwa serikali inaweza isishughulikie suala la katiba mpya na kuvifanya vyama hivyo kukosa wawakilishi bungeni na hata ruzuku, lakini anabainisha kuwa hatua hiyo itakuwa hailengi kuimarisha demokrasia, uwajibikaji na utawala bora.



Mjumbe wa JUKATA, Hebron Mwakagenda. **PICHA: MTANDAO**

Mchambuzi huyo anafafanua kuwa, kuna mambo matatu muhimu ambayo Rais ana uwezo nayo kwa ajili ya kuwapa Watanzania nayo ni katiba mpya, kuweka usawa wa kijinsia katika uongozi na kushughulikia kero za muungano.

"Rais alikuwa Makamu Mwenyekiti wa Bunge Maalum la Katiba, hivyo suala la katiba mpya analijua vizuri, amekuwa Waziri na Makamu wa Rais hivyo kero za Muungano anazijua amalize yote hayo," anasema.

Anaongeza kuwa , suala la usawa wa kijinsia katika uongozi, hana mashaka nalo, kwa kuwa Rais ameanza kuonyesha nia kuhakikisha anateua wanawake wengi katika nafasi mbalimbali kwenye serikali yake.

### UMAKINI NI MUHIMU

Mwenyekiti wa Taasisi ya Utawala Bora na Maendeleo Tanzania (CEGODETA), Thomas Ngawaiya, akitoa maoni yake anasema, katiba ni muhimu kwa manufaa ya Watanzania wote, lakini pia anaongeza kuwa si vizuri vyama kususa uchaguzi mkuu kwa sababu ya madai hayo.

"CHADEMA na CUF wanatakiwa kuendelea kudai katiba mpya huku wakishawishi Watanzania kujua umuhimu wake, kwani wakisusa haitawasaidia, vyama vingine vitashiriki," anasema Ngawaiya.

Anasema, kuna vyama vingi vya siasa vyenye usajili wa kudumu, ambavyo kila kimoja kina mtazamo wake, na kwamba kuna uwezekano CHADEMA na CUF vikasusa, lakini vinatoa nafasi kwa vingine kupata umaarufu.

"Sikatai vyama hivyo vikubwa kudai katiba mpya, ila ushauri wangu ni kwamba vifanye hivyo huku vikiendelea kushiriki uchaguzi, vinginevyo vitajikuta vinapoteza wanachama na mashabiki," anasema.

Anasema, chama kinaposhiriki uchaguzi na kupata madiwani na wabunge, kinajiongezea umaarufu na kujitanua zaidi, na kwamba kikijiweka pembeni kuna uwezekano mkubwa wa kukimbiwa na wapenda mageuzi.

### KUIMARISHA DEMOKRASIA

Mkurugenzi Mtendaji mstaafu wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) cha Dar es Salaam, Dk. Hellen Kijo Bisimba, anasema kuna haja kwa serikali kukaa na kutafakari kwa kina na kisha, kwa nia nzuri ya kuimarisha demokrasia nchini.

"Kwa kuwa ushiriki wao ni muhimu sana kwa mustakabali wa demokrasia kama tunaijali hiyo demokrasia, tuna miaka minne ya kutekeleza wayatakayo ili waweze kushiriki katika uchaguzi mkuu," anasema Dk. Kijo-Bisimba.

Mwanasheria huyo anasema, vyama hivyo visiposhiriki katika uchaguzi, ni hasara kwa demokrasia na kwamba, kama nchi, itakuwa imepoteza kile ambacho dunia inakisisitiza nacho ni demokrasia.

"Katiba mpya si kwa manufaa ya vyama vya siasa tu bali ni kwa Watanzania wote, hivyo ni muhimu wote kudai uwepo wa katiba mpya kwani uchaguzi ukiwa ni wa chama kimoja tu ni hasara kwa Watanzania wote," anasema.

Anafafanua; "Tanzania si kisiwa bali ni sehemu ya dunia inayotutegemea tuwe katika hali fulani, kukosekana kwa demokrasia kutatutenga na ulimwengu na tutakosa nyenzo muhimu za kuwajibishana kuelekezana kwa maendeleo ya nchi yetu kwa ujumla."

### KILIO KILIPOANZIA

CUF na CHADEMA, vilitangaza rasmi kwamba, kuanzia sasa havitashiriki uchaguzi mkuu wa mwaka 2025 hadi kwanza kuwe na katiba mpya na tume huru ya uchaguzi.

Novemba mwaka jana, Mwenyekiti wa CUF Taifa, Profesa Ibrahim Lipumba, alitangaza kuwa chama hicho hakitashiriki uchaguzi wowote na badala yake kitajikita katika harakati za kudai katiba ili tume huru ya uchaguzi ipatikane, lakini pia akamweleza John Magufuli, wakati wa uhai wake , alipokutana na wadau wa haki za binadamu na sheria kwe-

INAENDELEA UK. 12



Rais wa Sudan Kusini, Salva Kiir, nchi yake inatikisa kwa mauaji ya wauguzi na madaktari wanaosaidia wagonjwa vijijini. **PICHA: MTANDAO.**

## AFRIKA

# S/Kusini yawa kaburi madaktari, na wauguzi wanaotoa misaada

**Na Michael Eneza**

MADAKTARI na wauguzi wa jumuia ya kimataifa wanaofanya kazi Sudan Kusini hasa chini ya kundi la Madaktari Wasio na Mpaka (MSF), wanaendelea kujitafuta au kujiuliza kama waendelee kufanya kazi ya kusaidia jamii iliyo katika janga la vita, umaskini na maradhi Sudan Kusini.

Ni kutokana na mashambulizi ya maharamia ambayo mara kwa mara yanalenga vituo vya afya, na kama ilivyotokea hivi majuzi, kuua daktari ambaye hata hivyo ni raia wa nchi hiyo. Matukio hayo yamezagaa maeneo tofauti na daktari huyo aliuawa jimbo la kaskazini la Unity wakati muuguzi aliuawa katika jimbo la Equatorial , wote mwezi uliopita.

Taarifa zinasema madaktari walitoa tahadhari ya mgomo baada ya mwenzao kuuawa Mei 21 mwaka huu, wakati matukio ya mashambulizi yakiongezeka. Aliuliwa eneo la Eastern Equatorial, kusini mashariki ya nchi hiyo.

Umoja wa Madaktari wa Sudan Kusini (SSDU) ulieleza kushtushwa kwake na mauaji hayo, ukimtaja daktari aliyeuawa kuwa ni Dk Louis Edward Saleh aliyekuwa akisaidia wakazi wa kijiji cha Ganyiel katika jimbo la Unity.

Maofisa wa Umoja wa Mataifa wanasema Sudan Kusini ni nchi hatari kwa madaktari na wauguzi kwa vile wauguzi kutoka nje takriban tisa waliuawa nchini huo mwaka jana, idadi ambayo haitaji raia wa nchi hiyo wanaofanya kazi pamoja na wageni hao ambao nao wameuawa.

Baadhi ya wafuatiliaji wa habari wanasema kuwa licha ya kuwa mashambulizi katika vituo vya afya na kuua au kujeruhi madaktari na wauguzi yanastusha zaidi, kwa jumla wafanyakazi wanaotoa misaada ya nje walioko Sudan Kusini muda wote wako katika hatari ya kushambuliwa.

> Haikuelezwa ni kiasi gani cha misaada kilichoibwa au wafanyakazi wa mashirika ya misaada kunyang'anywa fedha, kwani makundi mengi ya waasi wanawalenga...

Januari mwaka huu, mfanyakazi wa kundi la kusimamia misaada ya aina mbalimbali linaloitwa Joint Aid Management (JAM) aliuawa katika jimbo hilo la Unity, huku Shirika la Msalaba Mwekundu (IRC) likibaki kimya kuhusu kuuawa kwa Dk. Saleh, na wizara ya afya jimboni humo ikisema kuwa uchunguzi wake umeanza.

SSDU ilitoa tahadhari ya hali ya hatari kutokana na vitisho, kupigwa, kukamatwa na kutupwa rumande, kuteswa na kuuawa kwa baadhi ya madaktari na wauguzi katika matukio ya mara kwa mara, Mapema mwezi uliopita mfanyakazi wa misaada aliuawa wakati msafara wa magari ya shehena ya misaada ulipshambuliwa kwa risasi magharibi ya nchi hiyo.

Haikuelezwa ni kiasi gani cha misaada kilichoibwa au wafanyakazi wa mashirika ya misaada kunyang'anywa fedha, kwani makundi mengi ya waasi wanawalenga wafanyakazi wa mashirika ya misaada ili wapindishe shehena ziende kwao, wazigawe.

Kimsingi ni kuwa jitihada ya kimataifa ya kuwasaidia wakazi wa maeneo tofauti ya nchi hiyo ambako athari za vita ya muda mrefu tangu Sudan Kusini imalize vita ya kujitenga na Sudan imalizike mwaka 2005. Tangu wakati huo watu wanaokisiwa kufikia 380,000 wamekufa katika makundi ya kisiasa na kikabila yanayohasimiana, au yanayonyang'anyana ng'ombe kwa mtutu wa bunduki na kutotambua utawala wa nchi au wa jimbo kama siyo wa kundi lililoko madarakani au lenye nguvu eneo husika. Licha ya kundi kubwa zaidi la upinzani kukubali kuingia serikalini Februari mwaka jana, silaha zimezagaa na hali ya uchumi haijatulia, hivyo wenye silaha wanatumia 'kula' kama ilivyokuwa Uganda ya Idi Amin.

Katika taarifa ya mwezi Aprili, mwaka 2018 asasi ya jijini New York inayofuatilia hali ya watoto katika nchi zilizogubikwa na vita ilisema vikosi vya majeshi ya serikali na vya upinzani vinashambilia vituo vya afya na kudhuru kwa makusudi watendaji kazi wa mashirika tofauti.

Asasi hiyo ilisema taasisi zisizopungua 50 zilishambuliwa miaka ya 2016 na 2017 na katika mashambulizi 750 ya wakati huo, makundi yenye silaha wakiwemo askari wa serikali yalizuia misaada kufikishwa mahali mashambulizi yalipotokea. Ni kwa mujibu wa mahojiano na madaktari na wauguzi 90 katika majimbo na Greater Upper Nile, Bahr el Ghazal na Equatoria. Christine Monaghan, mtafiti tangulizi wa asasi hiyo, alisema matokeo yake ni kuparaganyika kwa huduma za afya kutokana na uharamia, askari wakiharibu, kuchoma moto, kunyang'anya mali na kukalia kama kambi hospitali na zahanati tofauti nchini humo. Ni balaa tupu.

***MTANDAO WA ARABIYA NEWS***

# Katiba ni hitaji la taifa si la upinzani

**INATOKA UK. 11**

nye maadhimisho ya siku ya sheria duniani.

Profesa Lipumba kwa msisitizo anasema, yaliyotokea katika uchaguzi mkuu wa Oktoba mwaka jana, yanakifanya chama hicho kujiweka pembeni na kuanza kudai katiba mpya, kwa kuwa ndiyo suluhisho la kasoro na malalamiko mengi katika uchaguzi.

Ili kutimiza azma hiyo na kufanikisha uamuzi huo wa kususia uchaguzi, Mwenyekiti wa CUF anawaomba Watanzania wote wapenda haki kuungana na chama hicho kwenye ibada maalum ya kufunga na kuacha kula mchana Novemba mwaka jana.

Ibada hiyo ilikuwa ni kila Mtanzania kwa imani yake kuomba hukumu ya haki kutokana na kile kilichofanyika kwenye uchaguzi huo wa mwaka jana ambao CCM ilishinda karibu kata zote na majimbo yote ya uchaguzi Bara na Visiwani.

Katika kutaka mabadiliko, CHADEMA nayo imetangaza kuanza rasmi mchakato wa kudai katiba mpya, tume huru ya uchaguzi na uimarishwaji wa misingi ya utawala unaozingatia sheria, haki za binadamu na usawa, huku chama hicho kikisema, hakitashiriki uchaguzi mkuu wa mwaka 2025 kama masuala hayo hayatatekelezwa.

Hiyo ni kauli ya mwenyekiti wa taifa wa chama hicho, Freeman Mbowe, wakati wa uzinduzi wa oparesheni ya 'haki' yenye lengo la kusajili wanachama wapya kote nchini kidigitali.

Uzinduzi huo ulifanyika wiki iliyopita makao makuu ya kanda ya kaskazini, jijini Arusha, huku Mbowe akieleza kuwa CHADEMA ina zaidi ya wanachama milioni 10 kwa sasa.

UCHAMBUZI

# Mkataba AfCFTA ndivyo taifa litakavyonufaika

## •Dawa ya mazalia ya mbu kulitoa



Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje, Balozi Liberata Mulamula, majukumu yake ni pamoja na kushughulikia mikataba ya ushirikiano na masuala ya mtangamano wa Afrika .**PICHA: MTANDAO.**

**Na Gaudensia Mngumi**

TANZANIA inaelekea kuridhia Mkataba wa Bara la Afrika wa Soko Huria (AfCFTA) wakati wowote kuanzia Juni hadi Oktoba mwaka huu.

Itauridhia baada ya serikali kupata ridhaa ya bunge kwenye vikao vyake vinavyofanyika ndani ya mwaka huu, hizo ni taarifa za Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa.

Tanzania inachukua hatua hiyo baada ya mataifa 54 kati ya 55 ya Afrika kuusaini na mengine zaidi ya 35 kuuridhia mkataba huo utakaoziwezesha nchi kufanyabiashara bila vikwazo ikiwa ni jitihada za kuendeleza mtangamano wa Afrika.

Mtangamano utakaowafikisha wanachama wa Umoja wa Afrika (AU) kwenye Afrika Mpya 'the Africa We Want au Agenda 2063', unalenga kuwa na bara liliungana kikamilifu, lenye sarafu, soko, visa na pasi moja tena lisilo na mipaka.

Tanzania kusaini mkataba wa AfCFTA na sasa kuuridhia ni mkakati wa kuimarisha mtangamano kwenye eneo la biashara ambao ni muendelezo wa azma ya kutekeleza mikataba ya AU inayolenga kuifanya Afrika kuwa bora zaidi kwa manufaa ya Waafrika.

Itakumbukwa kuwa Tanzania iko kimya kwenye mkataba wa Afrika wa Demokrasia, Uchaguzi na Uongozi (ACDEG), hili nalo awamu ya sita inategemewa kuaridhia AfCFTA. Hata hivyo, haijausaini wala kuuridhia mkataba wa ACDEG.

Chini ya makubaliano ya AfCFTA Waafrika wanakusudia kuuza kila walichonacho bila vikwazo wala masharti magumu, kwa hiyo jukumu la Tanzania inayojiandaa kuuridhia ni kujihoji ni vipi itanufaika na biashara hiyo?

La muhimu ni taifa kujiandaa kikamilifu kuwezesha vijana na wanawake washiriki kufanyabiashara na zinazowanufaisha vinginevyo taifa litakuwa limechemka.

Inawezekana sekta binafsi Tanzania haina wafanyabiashara wengi wa ndani Idadi ya kinamama na vijana wanaoweza kushiriki kikamilifu kwenye AfCFTA ni ndogo, lakini ni lazima kuangalia eneo la kipaumbele na lile ambalo kama taifa linaweza kuwa mlango wa kuingilia kwa sababu ni masuala ya kimtangamano yasiyokwepeka.

Wakati serikali inasubiri saini ya bunge kuuridhia mkataba ni wakati wa kuhakikisha kuwa jukumu la kufanyabiashara kupitia mkataba wa Soko Huria la Afrika haunufaishi kampuni za kigeni au za kimataifa zilizoko nchini.

> Dawa za Biotech zinaweza kuwa eneo la kimkakati la kujitosa kwenye soko la AfCFTA kwa kuwa Tanzania ni nchi pekee barani Afrika yenye kiwanda hicho, vingine vitatu vinapatikana Japan ,Marekani na Cuba kwa mujibu wa taarifa za Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC) linalomiliki kiwanda hicho.

Tanzania ijitazame inakuwaje na inaanzaje kuingia kwenye soko hilo kwa kuwa kuna rasilimali nyingi na za kipekee za kuuzia mataifa mengine.

Chimbuko la makubaliano hayo ya kibiashara ni Kigali nchini Rwanda yaliyofikiwa Machi 21, 2018 wakati huo Mwenyekiti wa Umoja wa Afrika (AU), akiwa Rais Paul Kagame na tangu mwanzo, kinachokusudiwa ni kufanikisha kuwa na soko la watu bilioni 1.2 kutoka nchi 55 wanachama wa AU.

Licha ya faida lukuki kutajwa pasua kichwa inabakia kuwa Tanzania itanufaikaje na makubaliano hayo?

AfCFTA inataka kuwapo na punguzo la ushuru wa bidhaa zinazouzwa kwenye soko la Afrika nje na ndani ya mipaka ya nchi wanachama.

Ili kufikia lengo hilo ndiyo wakati wa kutekeleza azma ya kuwa na Tanzania ya viwanda ambayo wakati wa uhai wake John Magufuli, wakati analiongoza taifa alikuwa analisisitiza na kutaka nchi iwe na viwanda vya kimkakati ambavyo vitaliwezesha taifa kuwa na bidhaa mbalimbali.

Hicho ndicho kitakachoifikisha Tanzania kwenye soko la AfCFTA na mojawapo ya maeneo ni bidhaa za kipekee zinazozalishwa nchini.

Kwa leo dawa ya viuadudu vya mazalia ya mbu inayotengenezwa na kiwanda cha Biotech kilichopo Kibaha mkoani Pwani, inaweza kuwa kianzio.

Kiwanda hiki kipekee ni mwarobaini wa kuzuia malaria yanayoishambulia Afrika badala ya kupoteza mamilioni ya fedha kununua dawa kutoka nje kwa ajili ya kutibu ugonjwa huo ambazo kwa miongo mingi hazijaleta tija .

Dawa za Biotech zinaweza kuwa eneo la kimkakati la kujitosa kwenye soko la AfCFTA kwa kuwa Tanzania ni nchi pekee barani Afrika yenye kiwanda hicho, vingine vitatu vinapatikana Japan ,Marekani na Cuba kwa mujibu wa taarifa za Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC) linalomiliki kiwanda hicho.

Tanzania ipange namna ya kupenya Afrika kwa kuwa na kiwanda hicho pekee barani hapa kinachozalisha dawa hiyo muhimu duniani.

Pamoja na kiwanda hicho, kwa mujibu wa taarifa za kazi za utafiti zilizoko kwenye mtandao, zilizofanywa na Dk. Leonard Akwilipo, Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, mwaka 2003, Tanzania ina hifadhi kubwa ya kaolin iliyoko Pugu, Malangali na Chimala machimbo ya Pugu yakitajwa kuwa yanaweza kuwa makubwa kuliko mengine barani Afrika.

Tanzania wakati inajiandaa kujenga viwanda vya kutengeneza bidhaa za kaolin, ambayo pia huitwa China clay, inaweza kuwa mzalishaji mkubwa wa udongo huo Kusini ya Sahara, ambao una umuhimu kwenye kutengeneza vifaa vya ujenzi -masinki ya vyooni, rangi, pia huzalisha vyombo vya nyumbani kama vikombe, sahani, lakini ni bidhaa muhimu hospitalini ikizalisha muhogo unaotumika kufunga mifupa ya majeruhi iliyovunjika.

Kwenye nishati hutengeneza vikombe vinavyotumiwa kupunguza umeme kwenye nyaya na zaidi ya hapo ina mamilioni ya matumizi viwandani.

Ni baraka zaidi ikijenga viwanda vya kuzalisha bidhaa hizo ili zipatikane nchini na kwa ujumla soko hilo linafungua mlango wa ajira kwa vijana na maendeleo kiuchumi iwapo Tanzania inawekeza na kujenga uchumi wa viwanda unaozungumzwa kwenye majukwaa ya kisiasa kila siku.

Tanzania ni mashuhuri Afrika kwa bidhaa za kilimo hasa vitunguu vyenye ubora wa kipekee, ina dagaa wa aina yake wanaopatikana Ziwa Tanganyika na Nyasa. Wanahitajika kufungashwa na kuuzwa.

Ni taifa lenye bidhaa nyingi za vito kuanzia tanzanite, rubi, zipo sanaa za kuchonga hasa vinyago, za kusuka na vitu vingine vya kitamaduni vingi vinavyovutia watu kama mashuka ya Kimasai ambavyo vinaweza kuingia sokoni barani Afrika.

**CHA MUHIMU**

Ili Tanzania na Afrika inufaike na makubaliano ya AU ya AfCFTA la msingi ni kupiga vita na kutokomeza rushwa ambayo inakwamisha uzalishaji wa bidhaa za ndani ili kuzipa nafasi kampuni za kigeni na watu wachache kunufaika na mkataba huo.

Lakini pia, inahitajika ridhaa ya kisiasa, viongozi kujitolea na kusimamia utekelezaji wenye tija wa AfCFTA na kukomesha ufisadi, migogoro ya kimaslahi na upendeleo ili taifa linufaike.

# MSWATI III WA 'ESWATINI'

## ■Aliyekereka Swaziland kuitwa Switzerland
## ■Akaibadilisha jina bila kushirikisha raia

**Na Mwandishi Wetu**

MFALME Mswati wa III wa Swaziland, mwaka 2018 alibadili jina la taifa lake rasmi na kuachana na makovu ya ukoloni. Kwa miaka mitatu sasa linaitwa eSwatini, jina linalomaanisha "nchi ya Waswazi", katika lugha ya Kiswati.

Alibadili jina baada ya kuona kuwa kutamka Swaziland ni kazi na watu wengi wanaiita Switzerland.

Mfalme Mswati anayejulikana pia kama 'Ngwenyama' kwa lugha ya taifa hilo jina likiwa na maana ya simba, anasifika duniani kwa kudumisha utamaduni akiendeleza mila ya kuoa wake wengi, kila mwaka.

Kiongozi huyo anajichagulia kimwana kwenye sherehe inayofahamika kama 'reed dance' ambayo ni ngoma ya mabinti wanaojikusanya mbele ya Mswati ili kujaribu bahati yao, kwa vile mmoja wao anachaguliwa kuwa mke wa Mfalme.

Watetezi wa haki za binadamu na za wanawake wanapinga utaratibu huo, wakisema kuwa ni udhalilishaji na unawalazimisha wasichana kujipanga mbele ya Mfalme kujionyesha na kama jamii zinawakataza mabinti kushiriki, hutozwa faini ya mifugo.

Iwapo msichana hataonekana kwenye sherehe hizo familia yake hupigwa faini ya beberu au dume la ng'ombe.

Itakumbukwa kuwa Aprili 2018 Mfalme Mswati wa tatu, alitangaza kubadilisha jina la taifa hilo, akieleza kuwa sababu kuu ya kubadilishwa kwa jina la nchi yake ni watu kuichanganya na Switzerland kila aendapo katika mikutano ya kimataifa.


Mswati alitangaza mabadiliko haya wakati taifa hilo la kusini mwa Afrika likiadhimisha miaka 50 tangu lijinyakulie uhuru kutoka kwa Muingereza na kuwaeleza `raia wake kuwa utaitwa "Ufalme wa eSwatini".

Alianza kampeni za kubadili jina mara kadhaa katika miaka hiyo wakati akihutubu kwenye mkutano mkuu wa Umoja wa Mataifa mwaka 2017 na pia katika kusanyiko la Umoja wa Afrika (AU) jijini Addis Ababa na makongamano mengine ya kimataifa.

Mswati wa tatu akihutubia umati mkubwa katika uwanja wa mji wa Manzini, kilomita 40 mashariki ya mji mkuu wa Mbambane, Mfalme alisema Swaziland ilikuwa inarudisha jina lake la asili ambalo lilikuwa linatumika kabla ya kutawaliwa na Uingereza.

Taifa hilo dogo la kifalme Kusini mwa Afrika ni mwanachama wa Jumuiya ya Madola na lilipata uhuru wake kutoka Uingereza mwaka 1968. "Ningependa kutangaza kuwa, kuanzia leo, taifa hili litafahamika kama eSwatini," mfalme aliwaambia raia.

Akisisitiza hoja ya kubadili jina anasema: "Jina la Swaziland limesababisha sintafahamu. "Kila wakati tunapozuru nje ya nchi watu wanasema tunatokea Switzerland ..."



Mfalme Mswati katika shughuli za kitaifa. **PICHA: MTANDAO.**

Anatangaza hatua hiyo akiwa amevalia mavazi ya kijeshi ya rangi nyekundu na nyeusi na kusafiri kwenye gari ambalo la wazi, alisema anachotaka ni kuona taifa lake likiwa na jina ambalo watu wake wanaweza kutambuliwa nalo na siyo kuhusishwa na majina ya mataifa yaliyoko Ulaya, akimaanisha Switzerland.

Hata hivyo, tatizo la mataifa kuchanganywa majina haliko Swaziland pekee hata 'Tanzania', baadhi ya watu duniani, huuita 'Tasmania' ambacho ni kisiwa kilichoko Australia kinachojulikana wakati mwingine kama Tassie au Bruny.

Siyo Swaziland pekee iliyobadili jina wakati huo, tena ikijibatiza upya mwaka 2018 kwani mwaka 2019 bunge la Masedonia taifa lililo jirani na Ugiriki lilipitisha mabadiliko ya katiba ili kuruhusu kubadilisha jina la nchi hiyo kuwa Jamhuri ya Mesedonia ya Kaskazini.

Tofauti kati ya Masedonia na Swaziland inakuwa ni maamuzi ya mfalme peke yake aliyeamua kubadili jina la Swazi na kuliita Ufalme wa eSwatin na kulitangulia bunge.

> Taifa hilo dogo la kifalme Kusini mwa Afrika ni mwanachama wa Jumuiya ya Madola na lilipata uhuru wake kutoka Uingereza mwaka 1968...

Hata hivyo, raia wengi walitaka kiongozi huyo badala ya kuhangaika na jina angeshughulikia kwanza tatizo la uchumi kwa sababu watu wanaishi katika hali duni na wanateswa na umaskini.

Taifa hilo linaelezwa kuwa lina umaskini mkubwa, na jamii nyingi zimeathiriwa na maradhi hasa VVU.

Katika sherehe za kubadili jina la nchi hiyo, Rais wa Taiwan -Tsai Ing-wen alihudhuria hafla hiyo iliyofanyika April 2018.

eSwatini imedumisha uhusiano wake na Taiwan badala ya China na ilikuwa ni mara ya kwanza kwa Tsai kuzuru Afrika tangu kuchukua usukani wa taifa hilo mwaka 2016.

Kama mataifa mengine, Swaziland haikubadilisha jina lake baada ya kupata uhuru wake kutoka kwa Uingereza iliyoitawala kwa zaidi ya miaka 60.

Hatua ya kulibadilisha jina imekuwa ikijadiliwa kwa miaka mingi na wabunge kadhaa wakianza kuizungumza tangu mwaka 2015.

Mfalme Mswati aliyetawazwa mwaka 1986 akiwa na umri wa 18, anadaiwa kutawala kwa mkono wa chuma na mara nyingi amekosolewa kwa maisha yake ya anasa licha ya wananchi wake wengi kuishi katika umasikini.

Ni mpinga demokrasia aliyekataza vyama vya kisiasa vya upinzani baada kuvipiga marufuku kushiriki kwenye uchaguzi.

Wagombea ambao wameidhinishwa na machifu pekee na waliootwatiifu kwa mfalme huyo, ndiyo wanaoruhusiwa kushiriki kwenye uchaguzi.

Taifa hilo lenye idadi ya watu takribani milioni 1.3 kubadili jina kulimaanisha kuwa katiba ya nchi hiyo ingerekebishwa halikadhalika mabadiliko yangefanywa kwenye idara za polisi, jeshi la ulinzi na Chuo Kikuu cha Swaziland.

Licha ya Swaziland kuchelewa, baada ya uhuru, nchi za Afrika zilibadili majina yake mfano, Rhodesia ilibadilishwa kuwa Zimbabwe, Nyasaland ikawa Malawi, na Bechuanaland ikawa Botswana.

Zambia ikazaliwa kutoka Northern Rhodesia, wakati Upper Volta, ilibadili jina na kuitwa Bourkina Fasso, ikimaanisha 'ardhi ya watu waadilifu.

**MTANDAO WA DW**



# Wanaokaidi kusafisha mashamba kuondolewa umiliki

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

NAIBU Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, amemuagiza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino kuwaondoa wamiliki 86 waliokaidi kusafisha maeneo yao kwenye shamba la ushirika la kilimo cha zabibu la Chabuma.

Shamba hilo lenye ukubwa wa ekari 600, kati ya hizo 300 zipo kwenye mfumo wa kisasa wa umwagiliaji.

Akizungumza katika ziara yake ya kukagua mchakato wa kulifufua shamba hilo lililoanzishwa mwaka 2008/9, Bashe alisema shamba hilo liliacha kuzalisha mwaka 2015 na alipolitembelea awali aliagiza wamiliki kusafisha maeneo yao ili kufufua kilimo hicho.

"Nilishatoa muda kila mtu asafishe shamba lake, lakini kuna watu 86 hawakuonekana na hawajasafisha, pia kulikuwa kuna watu wakubwa wanamiliki mashamba, naomba muwaondoe na mashamba hayo yagawiwe kwa wakulima wengine ambao wapo 'serious' kwa ajili ya kushirikiana katika safari ya kulifufua shamba hili," alisema.

"Ninawaambia atakayenizuia kuwaondoa watu hao labda awe ni Rais Samia Suluhu Hassan, Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango na Waziri wangu wa kilimo, Prof. Adolf Mkenda, hao wanne tu ndio wanaoweza kunizuia kuwaondoa na hakuna mwingine maana maamuzi tulishafanya na tulishatoa muda, kama walifikiri tunafanya sanaa hapa."

Aidha, alisema awamu ya kwanza ya ufufuaji wa shamba hilo umekamilika na wanakwenda kuanza awamu ya pili.

Alisema katika shamba hilo kulikuwa kuna visima vitatu vya maji ambavyo vilikuwa vinatoa maji lita 40,000 hadi 50,000 kwa saa na bwawa linahifadhi lita 41,000 na wameanza kuvifufua.

Bashe alitoa siku 15 kuhakikisha kazi zote zinakamilika ili mradi huo uanze mwaka huu.

"Tulijiwekea lengo na wakulima hapa kwamba lazima mwaka huu shamba hili liamke na hatua za awali inatia moyo wakulima wameungana wanashinda wenyewe hapa shambani kwa kushirikiana na wataalam wa Wizara ya Kilimo kwa ajili ya kulifufua na kama mnavyoona tayari bwawa limesha karabatiwa na maji yanaingia," alisema.

Hata hivyo, Bashe alisema uwekezaji huo unaofanywa na serikali wakulima watarejesha fedha zote baada ya uzalishaji kuanza.

Alisema baada ya shamba hilo kufufuliwa watakaa na watu wa Shirika la Viwanda Vidogo (SIDO) ili watengeneze miundombinu itakayowawezesha wakulima kuuza mchuzi badala ya kuuza matunda yazabibu ili kilimo chao kiwe na tija.

Awali, akitoa taarifa ya ukarabati wa bwawa na visima katika shamba hilo, Mhandisi wa Tume ya Taifa ya Umwagiliaji Mkoa wa Dodoma, Raphael Laizer, aliiomba serikali iwasaidie fedha kwa ajili ya kununua vifaa vya kumalizia ukarabati.



Waziri wa nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Uratibu, Bunge,Vijana, Kazi, Ajira na Watu wenye Ulemavu), Jenista Mhagama (watatu kushoto), akikata utepe kuashiria kugawa vyerehani vilivyotolewa na Shirika la Mpango Chakula Duniani (WFP) kwa vikundi vya ujasiriamali vya Wilaya ya Chamwino, mkoani Dodoma juzi. (Watatu kulia) ni Mratibu wa Mradi wa Boresha Lishe wa WFP, Alessia Decaterina. **PICHA: RENATHA MSUNGU**

# Ujenzi nyumba NHC wafurahiwa na Kamati ya Ardhi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KAMATI ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii imeridhishwa na utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa nyumba 400 zinazojengwa mkoani Dodoma na Shirika la Nyumba la Taifa (NHC).

Mwenyekiti wa kamati hiyo, Dk. Aloyce Kwezi, aliyasema hayo juzi katika ziara ya kukagua ujenzi wa nyumba 300 katika eneo la Lyumbu na nyumba 100 wilayani Chamwino.

Alisema, kamati inaridhishwa ujenzi wa nyumba hizo kwa viwango vinavyotakiwa na hatua hiyo ni darasa kwa wajenzi wengine.

"NHC inatarajia kujenga nyumba 1,000 na leo tumetembelea 400, miradi hii kwa kweli inatakiwa kupongezwa ndiyo maana kamati yangu, imeanza kumpongeza waziri kwa kazi nzuri na kuwapongeza watendaji wake tumeona ubora wa miradi inayoendelea," alisema.

"Kwanza ni ubora, lakini la pili miradi hii ni shamba darasa kwa wajenzi binafsi pamoja na wajenzi wengine ambao watapenda kwa ajili ya kuikuza Dodoma yetu, lakini tutafurahi zaidi kwa sababu lengo ni miradi ikamilike kwa wakati halafu wananchi waje wapate huduma," alisema. Alisema wananchi wengi Dodoma ni wageni na wanahitaji nyumba, lakini zinauzwa kwa gharama kubwa na kwamba mradi huo utatoa nafuu kwao.

Kwa upande wake, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, alisema nyumba hizo zitakopeshwa kwa wananchi ikiwamo wafanyakazi wa serikali.

"NHC inatumia mradi huu kama shamba darasa kuwafundisha Real Estate namna bora ya kujenga nyumba imara bora, lakini pia kumekuwa na udhaifu kwa wauzaji wa nyumba ambao wamekuwa wakifanya udanganyifu kwa kuwauzia nyumba matokeo yake wafanyakazi wanalipa ya muda mrefu," alisema.

Waziri Lukuvi alisema serikali itamsaidia mnunuzi wa nyumba kupata mkopo benki wa nafuu ambao hautakuwa mgumu kwake kulipa.

Alisema mpango wa serikali ni kujenga nyumba katika kila eneo katika mikoa hapa nchini.

"Sisi Shirika la nyumba kwetu sisi kama Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa sekta ya nyumba tumeliteua Shirika la Nyumba kama kiongozi wa wajenzi wa nyumba hizi za makazi.

"Kwa kweli hatutaruhusu kununua nyumba zaidi ya moja na tutawajua tu, hatutaki nyarubanya hapa kwamba ununue zote halafu upangishe watu wote haiwezekani kwanza serikali imetoa fedha hizi ili mwananchi akopshwe kwa gharama nafuu."

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa NHC, Dk. Maulidi Banyani, alisema dhamira yao ni kujenga miradi mingi nchini kwa kuwa kuna ardhi ya kutosha.

"Sisi kama NHC yapo maeneo mbalimbali nchini tunadhamiria kujenga miradi ya namna hii ili tuweze kufanikisha haya ni lazima tuwe na ardhi na sisi kwa hivi sasa tuna ardhi katika maeneo mbalimbali kwa mfano, Mtwara, Mara, Lindi," alisema.

Alisema kwa Mkoa wa Dodoma wamefanya mazungumzo na Jiji la Dodoma na tayari wameishapata maeneo Mapinduzi na Mahoma kwa ajili ya awamu ya pili ya ujenzi wa nyumba maalum za viongozi.

"Kwa hiyo tumejiandaa na tunahakika kwamba miradi hii itaendelea kutekelezwa sehemu mbalimbali za nchi," alisema.

# 'Watoa huduma afya wapatiwe elimu lugha ya alama'

**Na Peter Mkwavila,** KONGWA

SERIKALI imeombwa kuwapatia elimu ya lugha ya alama watoa huduma za afya katika vituo vya afya na zahanati wilayani Kongwa, ili kuwahudumia na kuwatambua kwa usahihi makundi ya watu wenye ulemavu.

Rai hiyo ilitolewa na Mtabibu wa zahanati ya Mautya wilayani humo, Suzana Petro, alipokuwa akizungumza kwa niaba ya watoa huduma za afya kwenye mafunzo ya utoaji huduma jumuishi za afya kwa watu wenye ulemavu yaliyofadhiliwa na taasisi isiyo ya kiserikali ya Foundation for Civil Society.

Alisema elimu ya lugha ya alama inahitajika kufundishwa kwa kuwa itawasaidia katika kuwahudumia na kuwatambua watu wenye ulemavu.

"Tunaiomba serikali kutupatia fursa hiyo ya mafunzo ya lugha ya alama, ili waweze kuwahudumia ipasavyo kama wanavyo wahudumia watu wasio kuwa na ulemavu," alisema.

"Kwa mfano mtu mwenye ulemavu hawezi kuongea na wala hasikii na anaongea kwa ishara tu, anapohitaji kuhudumiwa kwa upande wetu tunalazimika kuomba msaada wa ukalimani ili tuweze kuwahudumia suala ambalo hatuwatendei haki makundi hayo ya walemavu."

Aliomba serikali kufanya marekebisho ya miundombinu ya baadhi ya majengo ya vituo vya afya na zahanati kwa kuwa siyo rafiki kwa makundi hayo ya watu wenye ulemavu.

Kwa upande wake, Katibu wa Shirikisho la Watu Wenye Ulemavu (SHIVYAWATA), Mkoa wa Dodoma Justust Ng'wantalima, alisema kuwa bado kuna unyanyapaa na ubaguzi kwenye vituo vya afya na zahanati hali inayowakatisha tamaa wanapougua na kushindwa kupata huduma ya kiafya.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Halmashauri ya Kongwa, Dk. Omary Nkullo, aliwataka wahudumu wa afya na zahanati kuonyesha upendo kwa vitendo kwa watu wenye ulemavu wanapowahudumia.

Alisema serikali inatambua watoa huduma za afya kwenye vituo na zahanati wengi hawana taalumu ya kutambua lugha hiyo ya alama na kutaka wasiwakimbie bali wahudumiwe.





# Washauriwa kutumia mapato kujiunga CHF

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

WANANCHI wilayani Chunya, mkoani Mbeya, wameshauriwa kutumia sehemu ya mapato yatokanayo na shughuli zao za kiuchumi ikiwamo kilimo na uchimbaji wa madini, kujiunga na Mfuko wa Afya ya Jamii ulioboreshwa (CHF) kwa ajili ya matibabu.

Ushauri huo ulitolewa juzi na Mkurugenzi Mtendaji wa wilaya hiyo, Sophia Kumbuli, wakati wa mkutano wa kusikiliza kero za wananchi katika Kata ya Mbugani wilayani humo kuwa gharama ya kujiunga na mfuko huo ni Sh. 30,000 kwa kila kaya.

Alisema wananchi wa wilaya hiyo huwa wanapata fedha nyingi hasa katika kipindi cha mavuno na kwamba ni muhimu wakajiunga na mfuko huo ili uwasaidie kwenye matibabu wakati wanapokuwa hawana fedha.

Alisema kwa lengo la serikali ni kuhakikisha wananchi wote wakiwamo ambao wapo kwenye sekta isiyo rasmi wanajiunga na Bima ya Afya ili kufikia lengo la afya bora na kwamba ni muhimu wananchi hao wakachangamkia fursa hiyo.

"Mfuko huu unakusaidia wewe na familia yako kutibiwa katika hospitali yoyote ya umma isipokuwa Hospitali ya Rufani, sasa naamini mnapata fedha nyingi sana kwenye shughuli zenu, unashindwa nini kutenga Sh. 30,000 kwa mwaka mzima kwa ajili ya kulinda afya ya familia yako?" Alihoji Kumbuli.

Alisema afya ndiyo msingi wa uzalishaji bora wa mali endapo mtu yeyote mwenye uwezo wa kuzalisha ama mtegemezi wake ataugua ni lazima shughuli za uzalishaji zitasimama ili kuhangaikia afya ya mgonjwa husika. Kwa mujibu wa taarifa ya Mganga Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Dk. Salum Manyatta, mpaka kufikia mwezi Desemba 2020 ni asilimia 2.2 pekee ya wananchi wote wa mkoa huo ndiyo walikuwa wamejiunga.

Dk. Manyatta alisema Mfuko huo ulianza rasmi kutekelezwa katika mkoa huo Aprili 2019 na idadi kamili ya kaya zilizokuwa zimejiunga ni 8,949 zenye wanachama 37,528.

Alisema Halmashauri ya Busokelo ndiyo iliyokuwa inaongoza kwa kusajili watu wengi zaidi kwa kufikia asilimia 3.93, ikifuatiwa na Halmashauri ya Rungwe ambayo ilikuwa imesajili asilimia 3.15 huku Halmashauri ya Chunya ikishika nafasi ya tatu kwa kusajili asilimia 3.1.

Alisema Halmashauri ya Jiji la Mbeya ilishika nafasi ya nne kwa kuandikisha asilimia 2.51, ikifuatiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya ambayo iliandikisha asilimia 1.76, Halmashauri ya Mbarali asilimia 1.62 na ya mwisho ilikuwa ya Kyela iliyokuwa imeandikisha asilimia 0.62.

Alisema kazi ya uhamasishaji na uandikishaji wa wanachama wapya inaendelea katika halmashauri zote za mkoa huo na kwamba vifaa kwa ajili ya kazi hiyo vipo vya kutosha.

"Mkoa ulipokea simu 23, vitambulisho vya wanachama 3,050, vifungashio 3,050 pamoja na vitabu vya stakabadhi 850 kutoka GIZ ambavyo viligawiwa siku ya uzinduzi kwa kila Halmashauri kwa ajili ya kuanza zoezi la usajili, lakini pia Mkoa ulipokea simu 738 kutoka Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), kwa ajili ya maofisa waandikishaji," alisema Dk. Manyatta.

Kutokana na takwimu za Ofisi ya Mganga Mkuu wa Mkoa wa Mbeya kuhusu idadi ya kaya zilizojiunga na CHF iliyoboreshwa, zinahitajika juhudi kubwa za kuhamasisha ili wananchi wengi zaidi wajiunge na kufikia lengo la serikali.

## Vikundi 100 wanawake, vijana vyaanza kupata mikopo

**Na Nebart Msokwa,** RUNGWE

VIKUNDI 100 vya wanawake na vijana wajasiriamali katika halmashauri za Rungwe, Busokelo na Mbarali mkoani Mbeya, wameanza kupatiwa mafunzo ya usimamizi wa biashara ili kujikwamua kiuchumi.

Vilevile, mafunzo hayo yanalenga kupunguza ukatili wa kijinsia unaofanyika kwa wanawake na wasichana katika baadhi ya maeneo ikiwemo ukatili wa kiuchumi.

Hayo yalisemwa juzi na Mratibu wa Shirika lisilokuwa la Kiserikali (KWEICO), kupitia mradi wa Mwanamke Imara, Stewart Lukinda, wakati uzinduzi wa mafunzo hayo katika Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe na kuwa kwa vijana wanalenga kuwaelimisha njia bora za uendeshaji wa biashara.

Lukinda alisema Shirika la KWEICO kupitia mradi wa Mwanamke Imara, unatekelezwa katika mikoa mitatu ya Tanzania bara ambayo ni Mbeya, Njombe na Kilimanjaro na kwa kila mkoa ni halmashauri mbili pekee zinazonufaika na mradi huo.

"Mradi wa Mwanamke Imara unatekelezwa katika mikoa mitatu ya Tanzania ambayo ni Mbeya, Njombe na Kilimanjaro na kwa Mkoa wa Mbeya, mradi huu unatekelezwa katika wilaya za Rungwe na Mbarali," alisema Lukinda.

Alisema mradi huo unafadhiliwa na watu wa Marekani (USAid) na utadumu kwa miaka mitatu na kwamba hadi kukamilika kwa kwake vikundi 300 vya wanawake na Vijana vitakuwa vimefikiwa kwa mikoa husika.

Ofisa Biashara wa Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe, Philip Mwakibete, alisema mafunzo hayo yanatoa fursa kwa halmashauri kuwatambua wajasiriamali ambao watapatiwa vitambulisho vilivyo tolewa na serikali kwa lengo la kuchangia kodi.

Mwakibete alisema halmashauri hiyo kwa kipindi cha mwaka jana iliwapatia vitambulisho vya wajasiriamali zaidi ya 8,000 na kwa mwaka huu wanatarajia kuwasajili wajasiriamali kwenye mfumo rasmi ili watambulike kila sehemu hususani kwenye taasisi ya mbalimbali za kifedha na serikali.

"Kama halmashauri yetu itajitahidi kuwaunganisha wajasiriamali wetu kwenye makongamano ya kibiashara ili bidhaa zao litambulikane maeneo mengine tutawanganisha na TBS ili angalau bidhaa ziwe na ubora wa kutambulikana kiserikali," alisema Mwakibete.



Mratibu wa shirika lisilokuwa la kiserikali la KWEICO, Stewart Lukinda, akitoa mafunzo ya uendeshaji wa biashara kwa vikundi vya wajasiriamali wanawake na vijana wa halmashauri za Rungwe na Busokelo mkoani Mbeya jana. **PICHA: NEBART MSOKWA**

## RC ataka uwasilishaji taarifa za utekelezaji miradi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MKUU wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, amewataka wakuu wa taasisi zote za umma mkoani humo kuwasilisha taarifa za utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo kwenye ofisi yake kila baada ya miezi mitatu ili kurahisisha ufuatiliaji.

Alitoa agizo hilo juzi wakati wa kikao maalumu na wakuu wa taasisi mbalimbali za umma na kwamba kumekuwa na utaratibu wa baadhi ya taasisi hizo kutekeleza miradi bila ofisi yake kujua jambo, alilosema ni kinyume na taratibu.

Alisema utaratibu huo utasaidia taasisi hizo kuepuka baadhi ya matatizo yanayoibuka kwenye miradi hiyo ikiwamo ufisadi na utekelezwaji wa miradi chini ya kiwango.

Alizitaka taasisi hizo kuainisha miradi yote iliyotekelezwa na kuwasilisha ofisini kwake ili iliyokwama ijulikane na sababu zake na iliyokamilika izinduliwe na kuanza kufanya kazi.

"Kama wewe ni benki tunataka utueleze umewakopesha wananchi wangapi, umefungua akaunti ngapi na thamani ya mikopo yako, lakini kama wewe unasimamia sekta ya maji unatakiwa utuletee taarifa inayoonyesha umetekeleza miradi mingapi, inanufaisha watu wangapi na iliyokwama ni mingapi," alisema Homera.

Alisema kwa miradi yote ambayo imekamilika na haijazinduliwa, viongozi wa taasisi hizo wanatakiwa kuandika barua na kuziwasilisha ofisini kwake wakiomba izinduliwe.

Baadhi ya viongozi waliohudhuria kilao hicho walizilalamikia baadhi ya taasisi kutekeleza miradi kwenye maeneo yao bila kuwashirikisha hali inayowapa wakati mgumu kwenye ufuatiliaji. Mwenyekiti wa Halmashauri ya Busokelo, wilayani Rungwe, Anyosisye Njobelo, alilalamikia Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA), kutekeleza miradi ya barabara bila kuwashirikisha akidai kuwa hali hiyo inasababisha wakose ushauri wa kuboresha.

Alisema hata katika ofisi za halmashauri hakuna taarifa sahihi kuhusu ujenzi wa miundombinu hiyo muhimu hali inayosababisha ugumu wa kuwaeleza wananchi.

"Tunataka watufafanulie, kwa mfano wanaweza wakatueleze kwamba Busokelo wamejenga barabara kadhaa zenye urefu kadhaa na kwa kiwango gani, hii itatusaidia kwenye ufuatiliaji, tunatakiwa tukienda tuzikute kweli hizo barabara," alisema Njobelo.

Naye Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Kyela, Katule Kingamkono, aliiomba serikali kutoa elimu vizuri kwa wananchi ili kuhakikisha wanakuwa na uelewa wa kutosha kuhusu miradi inayotekelezwa kwenye maeneo yao.

Alisema katika Wilaya ya Kyela kuna baadhi ya maeneo yenye matatizo kwa baadhi ya wananchi kugoma kupisha miradi ya maendeleo kutokana na kutoelimishwa vizuri kuhusu faida za miradi husika.

Mratibu wa TARURA wa Mkoa wa Mbeya, Wilson Mwita, alisema katika mwaka wa fedha 2022/2023 bajeti zao zitaanza kupitishwa kwenye halmashauri ili kuondoa malalamiko ya madiwani kutoshirikishwa kwenye miradi.





# Bil. 200/- zasakwa ujenzi hospitali

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar (smz) imesema imeanza mchakato wa kutafuta fedha Sh. Bilioni 200 kwa ajili ya ujenzi wa hospitali ya kisasa ya rufani Binguni, wilaya ya Kati Unguja. Waziri wa Afya, Ustawi wa Jamii, Jinsia na Watoto, Nassor Ahmed Mazrui, alisema hayo jana wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Viti Maalumu, Mwanaidi Kassim Mussa, aliyetaka kujua lini ujenzi wa Hospitali ya Binguni utafanyika.

Alisema serikali kwa sasa imesitisha mpango wa ujenzi wa hospitali ya kisasa iliyoko Binguni na kazi kubwa inayofanywa ni kutafuta fedha kutoka kwa wafadhili mbalimbali kwa ajili ya kazi hiyo inayotarajiwa kufanyika kwa miaka mitatu.

Mazrui alisema SMZ tangu mwaka jana ilitenga bajeti ya Sh. bilioni sita kwa ajili ya mradi huo lakini fedha hizo hazikupatikana.

'Mheshimiwa Spika kwa mujibu wa maagizo ya Rais Dk. Hussein Ali Mwinyi, ametutaka tutafute fedha sehemu yoyote au tukopе Sh. Bilioni 200 na tujenge hospitali hiyo kwa muda wa miaka mitatu tu," alisema.

Alisema nia ya serikali kujenga hospitali hiyo ipo kwa sababu ni sehemu ya utekelezaji wa Ilani ya Ucuaguzi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2020-2025 yenye mikakati ya kuhakikisha inakuwa na hospitali kubwa iliyokamilika kwa ajili ya kutoa huduma za afya kwa wananchi.

"Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi msiwe na hofu ujenzi wa hospitali ya Binguni. utekelezaji wake upo na nimekabidhiwa jukumu la kutafuta fedha sehemu yoyote. Najua ujenzi wa hospitali hii ni sehemu ya utekelezaji wa ilani ya CCM ambayo mimi nimetakiwa kuitekeleza"alisema.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Zanzibar, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora, Haroun Ali Suleiman, akiwa na Ofisa Mtendaji Mkuu wa shirika la Legal Services Facility (LSF), Lulu Ng'wanakilala, wakizindua rasmi Wiki ya Msaada wa Kisheria mjini Zanzibar juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Ataka uongozi wenye maono

**Na Mwandishi Wetu,** PEMBA

MJUMBE wa Kamati Kuu ya Chama cha ACT Wazalendo, Othman Masoud, amesema Zanzibar inahitajika uongozi wenye maono na dhamira ya kweli ili kuikuza kiuchumi.

Aliyasema hayo Micheweni, Mkoa wa Kaskazini Pemba, katika Ukumbi wa Halmashauri akiwa katika ziara iliyoandaliwa na chama hicho kwa ajili ya kumtambulisha kwa viongozi wa mikoa, majimbo na matawi.

Othman ambaye pia ni Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, ameitaja Serikali ya Umoja wa kitaifa (GNU) na viongozi wake kuwa hatua muhimu ya kuelekea matarajio hayo.

Alisema kuwa mataifa mengi Duniani yameendelea kutokana na maono ya viongozi wake na kutolea mfano Singapore na kueleza kuwa isingeweza kuendelea bila ya uwapo wa viongozi wenye maono.

Pia aliema Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, ameonyesha maono katika kuinyanyua Zanzibar kiuchumi.

"Lakini kama atakuwa Rais pekee na wengine wakakosa maono ya maendeleo, basi tunamuumiza kifua na kuwa nguvu," alisema Othman.

Alisema Rais wa Zanzibar amekuwa akisisitiza maridhiano kwa sababu maono yake yanamwonyesha kuwa ili Zanzibar ipae kiuchumi, lazima uwapo umoja wa kitaifa

Othman alisema ni lazima kila mmoja awe na maono ya kuirudisha Zanzibar katika hatua ambayo ilifikia kiuchumi miaka ya 1960.

Alisema Zanzibar ilikuwa nchi ya tatu barani Afrika kiuchumi lakini leo imeshuka.

"Tumekuwa tukimsikia Rais wetu akiwatumbua wabadhirifu kwa sababu ameona wanamkwamisha katika juhudi zake za kuinyanyua Zanzibar kiuchumi," alisema Othman.

Alisema fikra hiyo itafikiwa ikiwa kila kiongozi atakuwa mwadilifu katika kutekeleza majukumu yake.

Kama viongozi watakuwa wanakwenda kinyume cha maadili ya utumishi wa umma, alisema itakuwa kikwanzo kikubwa kuwa na viongozi wenye maono ya kuinyanyua Zanzibar kiuchumi.

Alisema tayari Rais ameshawasimamisha viongozi wengi ambao si waadilifu katika nafasi ambazo wapewa.

Naye Makamu Mwenyekiti wa ACT Wazalendo Zanzibar, Juma Duni Haji, alisema umefika muda kwa masheha wa Zanzibar kufuta lawama ambazo hupokea kutoka kwa wananchi kutokana na kuwanyima vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi (Zan ID).

Alisema tayari Waziri husika amesema hadharani kuwa sheha yeyote atakayemnyima mwananchi kitambulisho hicho atachukuliwa hatua na kuhoji kwa nini Sheha akubali kuadhirishwa.

## Matumizi EFD sasa rasmi Zanzibar

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais Fedha na Mipango, Jamali Kassim Ali, amesema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inakusudia kuanza rasmi kutumia mashine za malipo ya kielektroniki na utoaji wa risiti (EFD) kwa wafanyabiashara Zanzibar kuanzia mwezi ujao ili kudhibiti mapato ya serikali.

Alisema hayo jana wakati akijibu hoja za wajumbe wa Baraza la Wawakilishi majumuisho ya michango ya makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka wa fedha 2021/22 katika kikao cha Baraza la Wawakilishi.

Kassim alisema wizara tayari ilikuwa imeanza kwa majaribio matumizi ya mfumo huo na kuwatambua wafanyabiashara wapatao 1,000 lakini ikabainika kwamba wako wafanyabiashara wajanja waliokuwa wakifanya udanganyifu ikiwamo kuingilia mtandao huo na kupotosha taarifa za takwimu.

Alisema maandalizi ya kuanza kutumia mfumo wa risiti za kielektroniki yamekamilika kwa kushirikiana na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) ambao wamekuwa wakitumia mfumo huo muda mrefu.

Pia aliwajulisha wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwamba serikali inakusudia kutumia mtandao wa ZAN-Malipo kwa wizara tano ambazo zimekuwa zikikusanya mapato.

Alizitaja wizara hizo kuwa ni Ujenzi Mawasiliano na Usafirishaji; Ofisi ya Rais Fedha na Mipango pamoja na Uvuvi na Uchumi wa Buluu.

Waziri huyo alisema serikali inaendelea na juhudi za kuimarisha miundombinu ya maeneo huru ya kiuchumi yaliyoko Micheweni kwa upande wa Pemba na Fumba Unguja ili kuwavutia wawekezaji.

Alisema maeneo hayo ni muhimu na yako kimkakati kwa ajili ya uwekezaji wa sekta za viwanda na miradi ya ujenzi wa hoteli za kitalii, ambayo ndiyo itazalisha ajira kwa vijana.

"Mheshimiwa Spika maeneo huru ya uchumi yaliyoko Fumba na Micheweni hayajatelekezwa. Tutayaendeleza kwa ajili ya kuweka miundombinu ya barabara, maji safi na umeme kwa ajili ya kuwavutia wawekezaji," alisema.

Alisema kwa mwaka wa fedha 2021/22 Ofisi ya Rais Fedha na Mipango, inatarajiwa kukusanya Sh. trilioni 1.78 ambazo ni ongezeko la asilimia 15 ikilinganishwa na makadirio ya Sh. trilioni 1.549.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya**
**NYALIKUNGU (W) MASWA**
**Usimamizi wa Mirathi Na 8/2021**

Ombi la **JUMANNE OMARY HAJI** kuteuliwa
Msimamizi wa mirathi ya marehemu **MARIAM OMARY JUMANNE NWL.ISANGA SHULE YA SEKONDARI-MASWA**
Kwa **YEYOTE ANAYEHUSIKA POPOTE PALE ALIPO**
Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na Mirathi ya marehemu huyo wanaalikwa kuja kuhudhuria kesi wakitaka mnamo **tarehe 28/06/2021** kabla huyo nwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo

---

**GN NO, 388 (Contd.....)** **FORM NO, 8/4**

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**JUDICIARY**
**IN THE DISTRICT COURT OF**
**AT MUSOMA**
**CIVIL CASE NO: 8, 2018**
**SADICK K.CHIGUMA...........PLAINTFF**
**VS**
**JONATHAN PETER MAPIGANO.........DEFFEN-DANT**
**Summons for Senttlement of Issue**
**(Order XIV, rule 1 & 2 of the Civil Procedure Code)**
**To: Jonathan P. Mapigano**
**P.O BOX 1872, MUSOMA.**

**WHEREAS** the above named plaintiff (s) has/have instituted as suit/Bill of Costs against you, you are hereby summoned to appear in this court in person, or by an advocate dully instructed, and able to answer all material questions relating to the suit, or who shall be accompanied by some person able to answer all such questions on the 11th, June, 2021 at 09:00 HRS in the forenoon/afternoon to answer the claim, and you are directed to produce om the day all the documents upon which you intend to rely in support of your defence to file on or before that date your written statement.
**TAKE NOTICE THAT** in default of your appearance on the day before mentioned, the suit will to bearsa and determined in your absence.
**GIVEN BY MY HAND AND THE SEAL OF THE COURT this 7th day of JUNE, 2021.**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI FORM II**
**(S.M.M. 1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)**
**Katika Mahakama ya Mwanzo MJINI MOROGORO**
**Usimamizi wa Mirathi NAMBA 162/2021**

Ombi la **SARAH MOHAMED MADUNDA** kuteuliwa Msimamizi wa mirathi ya marehemu **SOLOMON EMANUEL MGHUMBA.**

Watu wote wanaodai kuwa uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaalikwa kuja na kuhudhuria shauri mnamo **tarehe 05/07/2021** kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo. Wosia wa marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa.

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**JOHN MUSSA BAMBA** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI YENYE NAMBA ZA USAJILI **T 715 ABY** – TOYOTA **HILUX**. YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI. TAARIFA YA POLISI: **DAR/OST/RB/ 288896/2021.**

---

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**
**Katika Mahakama ya Mwanzo**
**MJINI MOROGORO**
**Usimamizi wa Mirathi**
**NO.172/2021**

Ombi la **RASHIDI ABDU ISMAIL** Kuteuliwa msimamizi wa mirathi ya marehemu **ISAYA YASINI JUAKALI**
Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaalikwa kuja kuhudhuria shaurini mnamo **tarehe 12/07/2021** kabla huyo mwambaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Wosia wa marehemu huyo upo hapa mahakamani waweza kukaguliwa.
**Tarehe 07/06/2021**

---

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**BEATRICE PETER KANY, Anatangaza kupotelewa na kadi ya Bajaji Yenye namba za usajili T 140DZ. Yenye Chassis namba AZR600403224 na Injini namba AZ510890. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Polisi Taarifa : BNG/RB/118/2021**

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**SRS CAR RENTALS LIMITED** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **TOYOTA RAV 4** yenye namba za usajili **T 187 DDH** chasis namba **SXA160025114** engine namba **3S7412485,**yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi Polisi taarifa **DAR/CEN/R-B/283094/2021**

---

## MNADA WA HADHARA

Kwa idhini tuliyopewa na **TUJIJENGE TANZANIA LTD, DEBT STAR & AUCTIONEER** tutauza kwa mnada wa hadhara Mali za wadaiwa Sugu kama ilivyotangazwa kwenye jedwali:-

| Mdaiwa | Mahali | Tarehe ya mnada |
|---|---|---|
| Naomi Joseph Wambura | Mbondole - Msongola-Ilala | 16.06.2021 |
| Abdul Hashim Said | Mbondole – Msongola-Ilala | 16.06.2021 |

Minada yote itafanyika mahali dhamana zilipo kuanzia saa nne asubuhi. Mteja atalipa 25% siku ya mnada, 75% atalipa ndani ya siku 14, akishindwa kulipa 25% iliyolipwa hailudishwi. Gharama za kubadili umiliki ni juu ya mnunuzi.

**Mawasiliano piga:**
**DEBT STAR: -**
**0782486826**
**0715486826**

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**LYDIA ALEXANDER MALEJEHE** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye jina la **DODOMA INNOVATION & PRODUCTION COM-PANY LIMITED** aina ya **CARDI TRAILLER** yenye namba za usajili **T 464 DDB Chassis No. ZB3773136FSU25110.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: DOD/-DOD/RB/244854/2021.

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo Wilaya ya Moshi**
**Kituo cha Uchira Mkoa Kilimanjaro**
**Usimamizi wa Na 6, 2021**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU NICHODEMUS. T. MACHA WA KAWAWA ROAD**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA LAURENCE. T. MACHA**
**TANGAZO**
**(Kanuni ya 5(2)ya usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote /maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 10 mwezi 6 mwaka 2021 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi ya hiyo .
Zingatia,
Endapo kuna yoyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa
* Wosia wa Marehemu huyo upo mahakamani na waweza kukaguliwa
* Marehemu hakuacha wosia
* Futa isiyo husika

**Imetolewa leo tarehe 13 mwezi 5 mawaka 2021**

..........................................
**HAKIMU**

---

**IN THE DISTRICT DELEGATE OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO.... OF 2020**
**In the matter of the Estate of the LATE TITUS GWASSAH**
**And**
**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY SIZYA TITUS**
**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of Probate Rules)**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before 30th Day of June 2021.
Dated at Dodoma this 20TH day of April 2021

..........................................

---

**JAMHURi YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI FORM II**
**(S.M.M 1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)**
**Katika Mahakama ya mwanzo MAKOLE**
**Usimamizi wa mirathi NA. 37/2021**
**Ombi la VERONICA GIDION LUGALA kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu RALPH WILLIAM MKUSA**

**KWA YEYOTE ANAYEHUSIKA NA MIRATHI HII POPOTE ALIPO**
Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya Marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnano tarehe 11/06/2021 kabla ya muombaji kuteuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa.
**Tarehe 31/05/2021.**

---

**OFISI ZA MATANGAZO**

**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**

**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

**Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku**




TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Kesi kutishia kuua kwa bastola yaahirishwa

**NA KULWA MZEE**

KESI ya kutishia kuua kwa bastola inayomkabili mfanyabiashara wa Kariakoo, Adelard Lyakurwa, imekwama kuendelea kusikilizwa kwa madai kwamba mshtakiwa ni mgonjwa.

Mahakama ya Wilaya ya Ilala jana ilitakiwa kuanza kusikiliza mashahidi wawili wa upande wa mashtaka mbele ya Hakimu Mfawidhi Martha Mpaze lakini ilikwama kutokana na mshtakiwa kutokuwapo.

Wakili wa Serikali, Nancy Mshumbusi, alidai kwamba upande wa Jamhuri una mashahidi wawili na wamefika mahakamani lakini mshtakiwa hayupo, anaumwa.

Mahakama iliwaonya mashahidi ili wafike kutoa ushahidi wao Juni 22, mwaka huu.

Katika kesi hiyo, Lyakurwa anashtakiwa kwa kumtishia kumuua kwa bastola mfanyabiashara maarufu Valence Lekule.

Mshtakiwa anadaiwa kutenda kosa hilo kinyume cha kifungu cha 89 (2)(a) cha Sheria ya Kanuni ya Adhabu Sura ya 16 iliyofanyiwa marejeo mwaka 2019.

Wakili Mshumbusi alidai katika maelezo ya awali kwamba Julai 30, mwaka jana, maeneo ya Kariakoo, mtaa wa Mbaruku na Swahili wilaya ya Ilala, mshtakiwa akiwa na lengo la kuua, alimtishia Lekule kumuua kwa kutumia bastola huku akijua kufanya hivyo ni kosa kisheria. Mshtakiwa anadaiwa kuwa ni mkazi wa Msasani na siku ya tukio la kutishia kuua, alikamatwa na kupelekwa Kituo cha Kikuu cha Polisi kwa tuhuma za kutishia kuua.

Mshtakiwa alikana maelezo yote kuhusu tuhuma zake lakini alikubali kwamba tarehe iliyotajwa alikuwa maeneo ya Kariakoo, mtaa wa Mbaruku na Swahili na Mei 12, mwaka huu, alikamatwa na kufikishwa mahakamani.

Baada ya kudai hayo, upande wa Jamhuri ulidai unatarajia kuita mashahidi saba katika kesi hiyo.

Wakili wa utetezi, Richard Mbuli, alishapewa maelezo ya mlalamikaji kwa ajili ya kufanya maandalizi ya kesi hiyo.

Mshtakiwa yuko nje kwa dhamana yenye masharti ya kuwa na wadhamini wawili waliokuwa na barua zinazotambulika kisheria na walitia saini dhamana ya maandishi ya Sh. milioni moja.



Wanafunzi wa Chuo kikuu cha Tumaini Dar es Salaam (TUDARCo), wakifanya usafi katika ufukwe wa Coco, eneo la Oysterbay jijini Dar es Salaam kama sehemu ya maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani mwishoni mwa wiki. **PICHA: FLORIDA RAYMOND WA TUDARCo**

# JATU yaanza kuuza hisa za bil. 7.5/-

**Na Mary Geofrey**

KAMPUNI ya Kilimo na Biashara ya JATU PLC, imeanza kuuza hisa zake milioni 15 zenye thamani ya Sh. bilioni 7.5 katika soko la hisa jijini Dar es Salaam (DSE) kwa lengo la kupanua kilimo nchini.

Kampuni hiyo imeshawanufaisha zaidi ya wanachama 32,000, huku ikiwa na lengo la kuwafikia Watanzania zaidi ya milioni 2.

Uzinduzi wa ununuzi wa hisa hizo umeanza baada ya Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA) kuidhinisha waraka wa matarajio wa kampuni ya JATU PLC kwa ajili ya kuuza hisa milioni 15 kwa Sh. 500 ulioanza Juni Mosi mpaka Julai 28, mwaka huu.

Uuzaji wa hisa hizo ni kutekeleza majukumu yake chini ya sheria ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (sura ya 79 ya sheria za Tanzania) na Mei 31, mwaka huu iliidhinisha waraka wa matarajio wa kampuni ya JATU PLC kwa ajili ya kuuza kwa umma katika soko la awali.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa ununuzi wa hisa hizo, Mkurugenzi Mtendaji wa JATU PLC, Peter Gesaya, alisema kampuni hiyo imeshafanikisha shughuli za kilimo katika maeneo mbalimbali, na kwamba wameshafikia hekari 70,000.

"Mpaka sasa tumeshafikia mikoa kumi na tumefanya kilimo cha machungwa, maparachichi, mahindi, alizeti, mpunga, ndizi na mboga, kwa maeneo yote tuliyozalisha unapata hekari 70,000, tunaamini kupitia kampeni yetu ya buku tano (Sh. 500) inatosha ambayo ni sawa na hisa 10 tutawafikia wananchi wengi zaidi," alisema Gesaya.

Asema kampuni hiyo imeamua kuingia kwenye soko la hisa ili kupanua kilimo na kuwasaidia wakulima kufanya kilimo chenye tija na kila mwanahisa atalima kulingana na hisa zake.

Alisema JATU PLC pia imepanga kuboresha miundombinu ya kilimo kwa kutoa pembejeo za kisasa za kilimo na mbegu.

# DC atoa siku saba malipo ya pango

**Na Zuhura Zukheir,** IRINGA

MKUU wa Wilaya ya Iringa, Richard Kasesela, ameagiza kutolewa notisi ya siku saba kwa wapangaji wa eneo la familia ya marehemu Rodrick Mahenge, kutokana na kugoma kulipa kodi huku akikanusha kuhusika kuchangia mgogoro wa familia hiyo na wananchi wa kijiji cha Isupilo na mwekezaji kampuni ya Overland.

Akizungumza kwa nyakati tofauti na viongozi wa Kijiji cha Isupilo, pamoja na familia ya Mahenge, Kasesela alisema kuwa tuhuma zinazoenezwa na baadhi ya wananchi kuwa yeye ni sehemu ya migogoro hiyo sio za kweli.

Alisema, kuhusu mgogoro wa familia ya marehemu Mahenge na wapangaji wake, baadhi ya watu wamemtengenezea tuhuma kuwa amejigawia eneo kwenye eneo hilo la familia.

Akizungumza na wasimamizi wa mirathi, Kasesela alisema lengo lake ni kuhakikisha anatatua mgogoro huo kwa amani na kuwaamuru wapangaji wote kulipa kodi na kuacha kuwa sehemu ya mgogoro wa familia.

Kasesera alisema kwa kuwa wamekuwa wasumbufu kulipa kodi na walishapewa notisi ya siku 30 hawajatekeleza, wapewe tena siku saba wahame kwa hiyari ili wawachie familia eneo lao.

"Hawa watu wamekuwa ni wakorofi hawataki kulipa kodi ya pango na wakapewa notisi ya kisheria ya siku 30 waondoke, lakini bado hawajatekeleza agizo hilo, mbaya zaidi wananiingiza mimi kuwa sehemu ya mgogoro niseme ninataka kuumaliza mgogoro huu kwa amani naomba ikatolewe tena notisi ya siku saba," alisema.

Kwa upande wake Jeny Mahenge, alisema kumekuwa na mgogoro wa muda mrefu baina ya familia na baadhi ya wapangaji kugoma kulipa kodi toka mwaka 2017 hadi sasa.

Alikanusha kuwa Mkuu wa Wilaya Iringa kumiliki eneo la marehemu Mahenge kama inavyodaiwa mitandaoni na mitaani.


Kwa upande wake Kasesela alisema alienda katika kijiji hicho kwa lengo la kutatua mgogoro huo uliokuwa umemfikia mezani kwake kama kiongozi na siyo kumpendelea mtu yeyote.

Alisema shamba la mwekezaji kampuni ya Overland lina hekari 1,262 huku 953 zikiwa hazina mgogoro wowote na 296 ndiyo zenye chanzo cha tuhuma hizo.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Kijiji cha Isupilo, Joachim Kisinini, alisema mgogoro upo kwa baadhi ya wanachi na mwekezaji.

Alisema kuwa shamba hilo lina hati ya mwaka 1929 na lilikuwa linamilikiwa na Rashid Kivike kwa kipindi chote hadi alipoamua kuliuza kwa kampuni ya Overland na kuibuka kwa mgogoro huo.

Alisema uongozi wa kijiji hicho hawaitambui hati hiyo kutokana na mmiliki wa awali kutolalamika mahali popote.




# RAIS PSG BADO AMTAKA MESSI

**PARIS, Ufaransa**

LIONEL Messi alitarajia kusaini mkataba mpya huko Barcelona msimu huu wa majira ya joto ili kumaliza uvumi juu ya hatma yake, lakini Rais wa Paris Saint-Germain, Nasser Al-Khelaifi, bado anajaribu kumshawishi raia huyo wa Argentina kutua Ufaransa.

Messi aliwasilisha ombi la uhamisho hapo Barcelona msimu uliopita wa majira ya joto, na bado hajasaini mkataba mpya na klabu hiyo huku mkataba wake wa sasa ukimalizika msimu huu.

"Ninachoweza kusema ni kwamba wachezaji wote wakubwa wanataka kuja PSG," Al-Khelaifi alisema katika mahojiano na L'Equipe.

"Haiwezekani kuwasajili wote, kwa sababu tayari tuna wachezaji katika kikosi chetu. Baada ya kusema hivyo, Messi ni Messi, mchezaji mzuri.

"Nimemwambia (Rais wa Barcelona Joan) Laporta kwamba, mkataba wa (Lionel Messi) unamalizika na kila klabu ina haki - kuanzia Januari Mosi - kufanya mazungumzo naye na ninaweza kumsajili kwa msimu huu wa majira ya joto."

# KANTE ANOGEWA KUKIPIGA CHELSEA

**LONDON, England**

KIUNGO wa Chelsea, N'Golo Kante, amesisitiza anafurahi kuwapo klabuni hapo na anataka kupata wakati zaidi kuendelea kushinda mataji mengi na 'The Blues' hao.

Kante ameelezea angefurahi kufanya hivyo kwa kusisitiza anajisikia 'vizuri' kuendelea kuwapo kwenye klabu hiyo yenye makazi yake jijini London.

Kiungo huyo amebakiza miaka miwili kumaliza mkataba wake pale darajani na inaelezwa kuwa Chelsea inataka kumuongeza mkataba kendelea kukitumikia kikosi hicho.

"Nimekuwa Chelsea kwa miaka mitano, nimefurahia misimu mizuri hapa," alisema Kante akinukuliwa na Jarida la France Football akiwa kambi ya timu ya Taifa ya Ufaransa.

"Natumai kuendelea kupata furaha ya ushindi zaidi pamoja. Sio kitu ambacho ninazingatia.

"Nina mkataba mwingine wa miaka miwili na Chelsea na ninajisikia vizuri na naamini kwamba nitaendelea kuwapo hapo."



# KOEMAN

## KASTAHILI KUPEWA MWAKA BARCA - GUARDIOLA

**BARCELONA, Hispania**

PEP Guardiola anaamini Ronald Koeman amestahili kubaki kama kocha wa Barcelona kwa msimu mwingine.

Koeman amebainisha alipata ahueni kuhusu majaliwa yake ya kuendelea kuwa kocha wa Barca wakati Rais Joan Laporta alipothibitisha kwamba ataendelea kuwa kocha kwa msimu wa 2021-22.

Koeman raia wa Uholanzi, aliiongoza Barca kutwaa taji la Kombe la Mfalme (Copa del Rey) msimu huu ulioisha na walimaliza nafasi ya tatu kwenye La-Liga, huku wakitolewa hatua ya 16 kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Na sasa mchezaji mwenzake wa zamani na Koeman hapo Barca, Guardiola, ametetea uamuzi wa kuendelea kumbakisha hapo kwa msimu mwingine zaidi.

"Koeman ataendelea kuwa kocha kwa msimu ujao, nilizungumza na Laporta na nina furaha kwamba rais alishawishika," alisema Guardiola akiiambia Cadena SER.

"Mimi ni rafiki mzuri wa Ronald. Ulikuwa mwaka mgumu kwa kila mmoja na Ronald anastahili mwaka mmoja zaidi, pamoja na watu uwanjani.

"Hata hivyo, mara zote mwaka wa pili unakuwa bora zaidi."



# GIROUD: NAWEZA KWENDA MILAN

**PARIS, Ufaransa**

MSHAMBULIAJI wa Chelsea, Olivier Giroud, amebainisha kuwa anaweza kuwa anajiandaa na kufikiria uwezekano wa uhamisho wa kuelekea AC Milan katika dirisha hili la uhamisho la majira ya joto.

Wiki iliyopita iliwekwa wazi kuwa mkataba wa Giroud umeongezwa kwa miezi 12 zaidi, ikionekana kama mpango wa kuelekea San Siro ndiyo umefika tamati.

Hata hivyo, Giroud, ambaye amezungumza na waandishi wa habari juu ya hatma yake, amesema Chelsea tayari walikuwa wameshapitisha suala la kuongeza mkataba wake mapema Julai, na wametangaza wiki iliyopita kwa sababu ya kuendana na sheria za EPL.

"Ni muhimu kukumbuka kuwa niliwapenda Marco van Basten na Andriy Shevchenko," alisema Giroud akiwaambia waandishi wa habari.


"Milan ni moja ya klabu kubwa Ulaya, lakini leo, sitazungumza juu ya hatma yangu na timu kwa sababu nimejikita kwenye mishemishe za timu ya Ufaransa na Euro, ambayo inakuja haraka.

"Lazima niseme wazi kuwa, kuna uwezekano nikajiunga na Milan, lakini kwa sasa siwezi kusema sana.

"Uwezekano ni mkubwa, kwa sababu sasa nataka kupata sehemu ya kucheza mara kwa mara, hivyo Milan naiona kama sehemu inayonifaa zaidi."

## COURTOIS AWEKA IMANI HAZARD KUBAKI MADRID

**MADRID, Hispania**



GOLIKIPA wa Real Madrid, Thibaut Courtois, anaamini kwa asilimia zote kuwa Eden Hazard atabaki klabuni hapo zaidi ya msimu huu wa majira ya joto.

Mchezaji huyo wa zamani wa Chelsea amekuwa na mwanzo mgumu kwa miaka miwili katika mji mkuu wa Hispania tangu alipojiunga na Real Madrid, akipata changamoto ya majeraha mengi yaliyomfanya ashiriki mechi 43 tu na kufunga mabao matano kwa klabu.

Hazard amekuwa akihusishwa kuungana tena na Chelsea na kumalizana na changamoto za muda wake aliokuwa huko Bernabeu, lakini Thibaut hatarajii kumuona akiondoka.

"Nina uhakika asilimai 100 atasalia. Hataki kuhama. Ni waandishi wa habari wa Madrid tu ndio wanaandika juu ya nia ya kuondoka."

Thibaut anasisitiza kuwa, Hazard anataka kupambana na kushinda akiwa na Real Madrid, bila kuwa na changamoto ya majeraha na kushinda mataji.

Hazard amekuwa akikosolewa zaidi tangu alipojiunga na Madrid kwa kiwango chake kuonekana kushuka tofauti na alipokuwa Chelsea.

## WHITE ACHUKUA NAFASI YA TRENT EURO 2020

**LONDON, England**



MLINZI wa klabu ya Brighton, Ben White, ametajwa kuwa mrithi wa nafasi iliyoachwa wazi ya Trent Arnold kwenye kikosi cha England.

White ameitwa kikosini hapo kuchukua nafasi ya Arnold baada ya kupata majeraha kwenye mechi ya kirafiki dhidi ya Austria mwishoni mwa wiki.

Nyota huyo alikuwa miongoni mwa wachezaji 32 wa kikosi cha awali cha wachezaji wa England walioitwa kabla ya kuchaguliwa wale 26 waliohitajika kuipambania kwenye michuano ya Euro 2020.

Nafasi iliyoachwa wazi na Trent ilionekana kama ingeweza kuzibwa na Jesse Lingard, James Ward au White.

Na sasa kocha Gareth Southgate ameamua kumpa beki huyo nafasi ili akasaidiane na Harry Maguire pale katikati.

Kitendo cha White kuchukua nafasi ya Trent kimeonekana kuwashangaza wengi kutokana na mategemeo ya wengi ambao walidhani itakuwa nafasi ya Lingard kutokana na mchezo mzuri alioonyesha kwenye ushindi dhidi ya Austria.

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# HALAAND ANUKIA KUTUA EPL, KUKIPIGA CHELSEA

●●●Abramovich yuko tayari kufadhili uhamisho huo kwa pauni milioni 154...

**LONDON, England**

CHELSEA imefanya mazungumzo rasmi na Erling Haaland juu ya hatua inayowezekana kumsajili kipindi hiki msimu huu wa majira ya joto, kwa mujibu wa ripoti ya vyombo vya habari vya Ulaya.

Mshambuliaji huyo wa Borussia Dortmund ndiye mali ya moto zaidi sokoni kwa sasa, huku Real Madrid, Barcelona na klabu za jiji la Manchester pia zikivutiwa naye.

Lakini 'Blues' hao wameamua kuingia mazima na mmiliki wake, Roman Abramovich yuko tayari kufadhili uhamisho wa pauni milioni 154.5 ambayo ni bei ya kuuliza ya Dortmund.

Kwa mujibu wa mwandishi wa habari, Kristof Terreur, hatma ya Haaland haitabiriki, ingawa alielezea mazungumzo kati ya washindi hao wa Ligi ya Mabingwa Ulaya na mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 20, yamefikia pazuri. Aliiambia The Football Terrace: "Najua kwamba kumekuwa na mazungumzo na watu wa Haaland hapo awali, lakini ni ngumu kutabiri pia.

"Kwa kweli, kwa kuwa Dortmund ilifuzu kwa Ligi ya Mabingwa, unahisi kuwa sasa wana sababu ya ziada ya kumbakisha.

"Lakini Haaland ndiye mchezaji ambaye kila mtu anataka kumpata na ningemsubiri."

Mwandishi wa habari wa Sky Sports Italia, Angelo Mangiante, aliunga mkono msimamo wa Terreur wiki iliyopita.

Ujumbe wake 'Tweet', ilisema kwamba Chelsea wamemfanya Haaland kuwa shabaha yao kuu, kwani Romelu Lukaku anaonekana kusalia Inter Milan.

## KWA UFUPI

**SANCHO SAFI UNITED**

MANCHESTER United wanakaribia kufikia makubaliano kumsajili, Jadon Sancho mwenye umri wa miaka 21, kutoka Borussia Dortmund baada ya bei ya winga huyo wa England kushuka hadi pauni milioni 80. ***(Times)***

**GUARDIOLA AMTAKA GREALISH**

KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola, anataka kumsajili kiungo wa kati wa Aston Villa na England, Jack Grealish mwenye umri wa miaka 25. ***(ESPN)***

**RONALDO BADO HAKIELEWEKI**

NYOTA wa Ureno, Cristiano Ronaldo mwenye umri wa miaka 36, anaelekeza darubini yake kwingine licha ya kufanya mazungumzo na Juventus kuhusu hatma yake katika klabu hiyo. ***(ESPN)***

**NUNO KUTUA EVERTON**

EVERTON wanaangalia uwezekano wa kumchukua kocha wa zamani wa Wolves, Nuno Espirito Santo, mwenye umri wa miaka 47, kurithi mikoba ya Carlo Ancelotti. ***(Football Insider)***

**ROMERO BEI YAKE HADHARANI**

KLABU ya Atalanta imeweka wazi kuwa bei ya nyota wao, Cristian Romero, mwenye umri wa miaka 23 raia wa Argentina kuwa ni pauni milioni 52. ***(Tuttosport)***

**EDOUARD AKARIBIA LEICESTER**

LEICESTER wamekubaliana na Celtic pauni milioni 15 kwa ajili ya mshambuliaji wa Ufaransa, Odsonne Edouard mwenye umri wa miaka 23. ***(Sun)***

**NEWCASTLE YAMTAKA CHOUDHURY**

NEWCASTLE wameingia kwenye mbio moja na Southampton katika za kumsajili kiungo wa kati wa Leicester, Hamza Choudhury mwenye umri wa miaka 23. ***(Football Insider)***

**JESUS KUMRITHI RONALDO**

ENDAPO Cristiano Ronaldo atahama Juventus, Gabriel Jesus mwenye umri wa miaka 24 kutoka Manchester City, anapigiwa upatu kuongoza katika orodha ya wachezaji watakaochukua nafasi yake.***(Gazzetta dello Sport)***

**PARKER ATAJWA BOURNEMOUTH**

KOCHA wa Fulham, Scott Parker, huenda akaondoka klabu hiyo ili kuwa kocha mpya wa Bournemouth. ***(Talksport)***

**WEST HAM, VILLA KWA WOOD**

WEST Ham na Aston Villa zinawania saini ya mshambuliaji wa Burnley, Chris Wood. ***(Mirror)***

**EKWAH ANUKIA WEST HAM**

WEST Ham wamefikia makubaliano ya kumsajili kiungo wa kati wa Chelsea, Pierre Ekwah mwenye umri wa miaka 19 raia wa Ufaransa. ***(Sky Sports)***



HABARI MICHEZO

# MAJALIWA ATETEA 'MAPRO' KUKIPIGA LIGI KUU NCHINI

**Na Abdallah Khamis, MTWARA**

WAKATI baadhi ya wadau wakiamini uwapo wa wachezaji wa kigeni nchini unawanyima fursa wazawa kung'ara, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Kassim Majaliwa, amesema badala ya Watanzania kufikiria kuacha kuwatumia 'mapro' hao katika ligi nchini, wanapaswa kujielekeza kwanza katika kukuza vipaji kuanzia ngazi ya msingi.

Aidha, amesema nyota wa kigeni wanaongeza ushindani kwa wachezaji wa ndani hali inayofanya michezo iwe na msisimko tofauti na kuwaacha wazawa peke yao.

Majaliwa alitoa kauli hiyo jana mkoani Mtwara, wakati wa ufunguzi wa mashindano ya Umoja wa Michezo na Taaluma kwa Shule za Msingi na Sekondari Tanzania (Umitashumta na Umisseta), ambayo kitaifa yanafanyika mkoani hapa, yakiwa na kaulimbiu ya "Michezo Sanaa na Taaluma kwa Maendeleo ya Viwanda na Uchumi".

"Tukiwaacha wachezaji kutoka nje, hatutakuwa na ushindani sahihi hususan katika soka kwa sasa, hivyo tuimarishe kwanza wachezaji wetu wa ndani kabla ya kufikiria kuachana na wa nje," alisema Majaliwa.

Aliongeza kuwa jamii haikuwaanda watoto ipasavyo kuwa wanamichezo imara wa siku zijazo, na kwamba ni wakati wa kubadilika ili matokeo ya michezo hiyo ya Umitashumta na Umisseta yaonekane.

"Serikali italivalia njuga jambo hili kuanzia ngazi ya chini kwa ajili ya kupata matokeo bora kwenye michezo na sanaa,"alisema Majaliwa Aliwataka washiriki wa michezo hiyo ya kutambua kuwa michezo ni ajira na wahakikishe wanatumia fursa hiyo kuonyesha vipaji vyao kwa ajili ya kuvutia wafuatiliaji wa vipaji vya michezo mbalimbali.

**Azipa wizara tatu angalizo**

Pia Majaliwa amezipa angalizo Wizara ya Habari, Utamaduni Sanaa na Michezo, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi na Tamisemi, kuhakikisha ari na msisimko ulioonyeshwa wakati wa ufunguzi wa michezo hiyo mkoani Mtwara haupotei kila mashindano hayo yanapofanyika.

Alisema wizara hizo zinapaswa kuhakikisha ushiriki wa michezo hiyo inakuwa endelevu wakati wote kwa kuwa inaipunguzia serikali gharama za kuwatibu watu wake kutokana na kutokufanya mazoezi

**Awaasa Wanafunzi**

Aidha Majaliwa aliwaasa wanafunzi wanaoshiriki michezo hiyo ya Umitashumta na Umisseta, watambue kuwa mpaka kufikia hatua hiyo wamepitia michakato mbalimbali kwa ajili ya vipaji walivyonavyo, hivyo wahakikishe hawabweteki.

Aliwaonya kutojiingiza katika matumizi ya dawa za kulevya kwa kuwa jambo hilo ni kosa kisheria, lakini pia huua vipaji vingi vya wanamichezo wanaochipukia

Alisema ni wakati wa kuwapata kina Mbwana Samatta, Kelvin John, Diamond Platnumz, Ali Kiba, Harmonize na kina Peter Msechu wengine watakaowakilisha Tanzania kimataifa katika nyanja mbalimbali za michezo na sanaa kimataifa.

MAANDALIZI...




Wachezaji wa timu ya Taifa, Taifa Stars, wakifanya mazoezi katika viwanja vya Jakaya Kikwete jijini Dar es Salaam jana, kujiandaa na mchezo wa kirafiki dhidi ya Malawi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Tiboroha: Yanga, Azam igeni Simba

**Na Adam Fungamwango**

KATIBU Mkuu wa zamani wa Yanga, Dk. Jonas Tiboroha, amezitaka timu zitakazokwenda kucheza mechi za kimataifa msimu ujao kuichukulia timu ya Simba kama kipimo endapo zinataka kufanikiwa na kufanya vizuri.

Tiboroha alikuwa akitoa maoni yake kama mdau wa soka kuhusu timu zitakazokwenda kuiwakilisha Tanzania kwenye mechi za kimataifa, ambapo pamoja na kuwa taarifa rasmi hazijatoka, lakini huenda nchi ikawakilishwa na timu nne msimu ujao.

Alisema klabu tatu ambazo zitakwenda kucheza mechi za kimataifa, ziiangalie kwanza Simba ni timu ya aina gani hapa nchini baada ya kwenda hadi robo fainali ya Ligi ya Mabingwa, lakini ikashindwa kutinga hatua ya nusu fainali, ndipo nazo zitengeneze timu yenye kariba hiyo kama zinadhamira ya kweli kwenda kushindana.

"Klabu zitakazokwenda kucheza kimataifa ziiangalie Simba ni timu ya namna gani. Imefikia hatua ya robo fainali na ikashindwa kupenya hatua ya nusu fainali, hivyo nazo zinatakiwa kutengeneza timu inayofanana kiuwezo na Simba au zaidi kama zinataka kufanya vizuri.

"Vinginevyo zitaishia hatua ya mwanzoni tu kwa kutolewa na timu za Etswatini na Comoro kwa sababu zitakuwa hazijafanya vitu vya msingi kujijenga," alisema.

Aliongeza kuwa Ligi ya Mabingwa na Kombe la Shirikisho ni michuano migumu ambayo inatakiwa kwanza kuwa na timu imara, kuwa na muda sahihi wa kujiandaa na si kujaribisha, lakini pia timu zinatakiwa kuwa vizuri kiuchumi, kwani ni michuano yenye gharama kubwa na kuna mambo yanahitajika pesa nyingi ili kuwa salama katika kukabiliana na baadhi ya vikwazo.

Timu za Simba, Yanga na Azam zina nafasi kubwa ya kuiwakilisha nchi kwenye michuano ya kimataifa; Ligi ya Mabingwa na Kombe la Shirikisho mismu ujao.

## Fomu ugombea Urais ZFF sasa hadi Juni 12

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

KAMATI ya Uchaguzi ya Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF), imeongeza muda wa uchukuaji fomu kwa wagombea wa urais wa shirikisho hadi Juni 12 bada ya jana ambayo ilikuwa siku ya mwisho.

Kuongeza kwa muda wa zoezi hilo ni ili kuwapa fursa wadau wa soka kujitokeza zaidi kuchukua fomu za kugombea nafasi hiyo.

Mpaka sasa waliochukua fomu za kuwania nafasi hiyo ni wagombea watatu ambao ni Abdulatif Ali Yasin ambaye ni Mwenyekiti wa Chama cha Soka Mkoa wa Mjini Magharibi, Suleiman Shabaan Suleiman, Mwenyekiti wa timu ya Chuoni FC na Suleiman Mahmoud Jabir, kocha na mkufunzi wa michezo Zanzibar.

Akizungumza na gazeti hili jana, Katibu wa Kamati ya Uchaguzi ya ZFF, Makungu Omar Makungu, alisema kiwango cha elimu kilichowekwa kwa wagombea urais ni shahada, ambacho ni kwa mujibu wa Katiba ya ZFF na kwamba hali ya mpira wa sasa duniani kote unaendeshwa kwa kutegemea zaidi elimu tofauti na uzoefu.

## Mechi za mwisho Ligi Kuu Z'bar zote Juni 11

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

BODI ya Ligi Kuu Zanzibar (ZBL), imetoa ratiba ya michezo ya mwisho ya ligi hiyo kwa msimu huu wa 2020/21.

Kwa mujibu wa ratiba hiyo iliyotolewa jana, inaonyesha michezo yote mitano itachezwa Juni 11, mwaka huu katika viwanja tofauti vilivyopo ndani ya mji wa Zanzibar na vile vya mikoani

Awali, ligi hiyo ilitakiwa kumalizika Juni 9, mwaka huu, lakini ZBL ililazimika kupangua ratiba hiyo ili kuepuka vitendo vya upangaji wa matokeo hususan kwa timu moja itakayoshuka daraja ambayo itaungana na Hard Rock iliyoaga mapema.

Michezo hiyo ya Juni 11, itachezwa katika viwanja vinne ambapo Mlandege itavaana na Malindi katika Uwanja wa Kinyasini mkoa wa Kaskazini Unguja huku Kipanga ikiwa na kibarua dhidi ya Mafunzo kwenye Uwanja Mau A uliopo Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja wakati Chuoni na JKU zenyewe zikipepetana katika dimba la Ngome lililopo Fuoni .

Mchezo kati ya Black Sailor na mabingwa wa ligi hiyo msimu huu, KMKM utachezwa Uwanja wa Amaan huku Polisi dhidi ya KVZ ukichezwa katika Uwanja wa Mchangani, mkoa wa Kusini Unguja.

# Michezo

Jumatano Juni 9, 2021

Nipashe




HALAAND ANUKIA KUTUA EPL, KUKIPIGA CHELSEA HABARI UK 22

UFUNGUZI...



Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, akikabidhi mmoja wa waamuzi mipira na filimbi, ikiwa ni ishara ya kufungua mashindano ya Umoja wa Michezo na Taaluma kwa Shule za Msingi na Sekondari Tanzania (Umitashumta na Umisseta), yanayofanyika Kitaifa mkoani Mtwara. **PICHA: Abdallah Khamis**

# TARIMBA ATINGISHA KUGOMBEA URAIS TFF

●●● Watu wengi wameniomba na wakunishauri kugombea, siwezi kusema...

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI fomu za kuwania nafasi mbalimbali katika uchaguzi mkuu wa Shirikisho la Soka nchini (TFF), zikianza kutolewa jana, aliyewahi kuwa Mwenyekiti wa Klabu ya Yanga, Abbas Tarimba, ametikisa mbio za kiti cha urais wa shirikisho hilo baada ya kuonyesha nia ya kutaka kuingia katika kinyang'anyiro hicho.

Kwa mujibu wa Mwenyekiti wa Kamati ya Uchaguzi ya TFF, Wakili Kiomoni Kibamba, uchaguzi huo utafanyika jijini Tanga Agosti 7, mwaka huu na nafasi zinazogombewa ni Rais wa TFF na wajumbe sita wa Kamati ya Utendaji, ambapo dirisha la kuchukua fomu lilifunguliwa rasmi jana huku likitarajiwa kufungwa Juni 12, mwaka huu.

Rais wa TFF anayemaliza muda wake, Wallace Karia, alishatangaza dhamira yake ya kutetea nafasi yake katika uchaguzi huo ujao, na huenda sasa akakutana na ushindani mkali kutoka kwa Tarimba.

Akizungumza jana baada ya tetesi za yeye kutia nia ya kugombea nafasi ya urais kuzagaa, Tarimba hakukubali wala kukataa, huku akieleza siku bado zipo za kutafakari uamuzi huo.

"Hizo taarifa zipo, watu wengi sana walikuwa wananiomba ama wananishauri, sijui kati ya haya mambo mawili, lakini watu wanalizungumza hilo suala. Siwezi kusema ndiyo ama hapana, lakini kama Mtanzania na kama wenzangu wananiona na mimi najiona kama nafaa, ila hadi sasa sijafanya uamuzi.

"Siku tano bado ni nyingi kama kutakuwa na uamuzi wa kuingia, tutaingia ama kama uamuzi utakuwa siyo kuingia basi hatutaingia, bado ninaendelea kupima," alisema Tarimba.

Kuhusu kuwa njiapanda kutokana na kushindwa kuweka msimamo wake wa kujitosa kugombea ama la, Tarimba alisema: "Hapana sipo njiapanda kwa kuwa suala ni uamuzi na muda, kwa sababu hili jambo limechipuka lazima tulifanyie uamuzi stahiki tuweze kuona ni jinsi gani tunaweza kuifanyia familia ya soka hapa Tanzania."

Tarimba mbali ya kuwa Mbunge wa Kinondoni, pia ni Mkurugenzi wa Uendeshaji wa Kampuni Michezo ya Kubashiri ya SportPesa Tanzania na amekuwa na mchango mkubwa katika soka la nchi hii.

Kwa kupitia SportPesa, kampuni hiyo ni wadhamini wa Klabu za Simba, Yanga na Namungo, lakini pia waliwezesha kufanyika ukarabati mkubwa wa Uwanja wa Benjamin Mkapa ikiwa ni pamoja na kuileta Klabu ya Sevilla ya Hispania kucheza mechi ya kirafiki dhidi ya 'Wekundu wa Msimbazi' hao.

## MKUDE, SIMBA SARAKASI MPYA

**Na Mwandishi Wetu**

HATIMAYE sakata la utovu wa nidhamu alilokuwa akituhumiwa kiungo wa Simba, Jonas Mkude na klabu yake, sasa linaonekana kugeuka kuwa sarakasi mpya, baada ya kutakiwa kwanza kwenda kupimwa afya kabla ya kushushiwa 'rungu' la adhabu.

Mkude alikuwa akituhumiwa kwa utovu wa nidhamu, kwa kutoripoti kambini na kutohudhuria mazoezini Mei 18, mwaka huu, lakini baada ya pande mbili kukutana, upande wa mchezaji huyo ukiongozwa na Wakili Tumaini Mfinanga na wa Simba ukiongozwa na Wakili Michael Mhina, kamati ikabaini makosa yanayomkabili yamekuwa yakijirudia rudia na amekuwa akitiwa hatiani na kupewa adhabu.

Hivyo, Kamati ya Nidhamu ya Klabu ya Simba chini ya Mwenyekiti wake, Suleiman Kova, ikaona ipo haja kwanza kumpeleka hospitali kubwa kwa wataalamu kwa ajili ya kumpima afya kwanza.

Akizungumza na mwandishi wetu, Kova alisema baada ya kusikiliza shauri hilo na kupata maelezo kutoka pande zote mbili, wameona waahirishe hukumu kwa sababu kumbukumbu za nyuma zinaonyesha amekuwa na tatizo la aina moja na la kujirudia mara kwa mara na kwamba hata yanafikishwa mbele ya kamati hiyo ni machache kwani mengi wanamalizana huko huko na viongozi wake.

"Tukaona kwamba huyu mtu anachohitaji kwa sasa si adhabu kwanza, ni msaada kujua tatizo lake ni nini ndiyo baadaye masuala ya adhabu yatakuja. Huu ni utaratibu tu wa kiuweledi, pia tuliangalia wenzetu nje ya nchi wanafanya nini kuna wachezaji wengi kama kina Georege Best waliwahi kupata matatizo kama haya, hivyo tulipoangalia nje tukaona ni busara zaidi tuwapelekee wenzetu ambao wanashughulikia na mambo ya tiba ya kisaikolojia, msongo wa mawazo ama jambo lingine lolote au gonjwa lolote ambalo ni sugu," alisema Kova.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002